BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,004,055,092/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SABAYA** kufanyiwa upasuaji kichwani, mshtakiwa mpya aunganishwa



MEMBE: SIBANDUKI TENA CCM HADI NIFE

Ukurasa 14

Ukurasa 13

siasa

JUMATANO JUNI 8, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

UCHAGUZI WA KENYA
Tume yapuliza kipenga

SAFARI YA MAPINDUZI KISIASA...

Maridhiano yanapoibua pongezi za Lissu, Mbowe kuteta na Rais Samia

- Historia ya yanayofanyika yatibu majeraha
- Simulizi za Unguja, Kenya kipekee marejeo

Na Peter Orwa

KIMSINGI, suala la maridhiano katika mustakabali wa kisiasa si jambo geni kwenye ulingo wa kisiasa na ndio imetawala katika sura nyingi ndani ya mataifa mengi, yakiwamo ya Afrika Mashariki.

Ikirejewa tafsiri ya kamusi ya Kiswahili nchini, mzizi wake unaanzia katika neno 'ridhia' ambayo kamusi hiyo inaorodhesha matendo kama: kutoa ruhusa kitu kifanyike, kubali, hiari na kuidhinisha.

Pia, ni tafsiri inayoenda mbali penye msamiati 'maridhio' unaobeba ufafanuzi:"Mambo ambayo mtu amekubaliana nayo." Kwa hilo, ndani ya siasa za nchi hasa awamu iliyopo ya uongozi wa kitaifa, ni jambo linaloendelea kuchukua sura pana katika mamlaka ya uongozi wa nchi, kukishuhudiwa hatua zake kwa yaliyo rasmi na yasiyo rasmi kufanyika.

Inaporejewa kwa kina kamusi ya kimataifa iitwayo Collins inayobeba tafsiri ya neno maridhiano kwamba ni: "Hali ambayo (watu) wanakubaliana na jambo ambalo liko katika mazingira halisi, au utashi wao, ili kuendana nayo sawa, au wanafikia utashi huo kutoa fursa ya kukubalika kwa utashi wa wenzake."

Nadharia za sayansi ya siasa na maandiko yake mbalimbali yanagusa dhana kwamba, ili kuwepo mafanikio na ubora wa utawala kisiasa, kuna ulazima mambo kadhaa yakajumuishwa uwepo wake yakiwamo; utawala uliopo ukubalike kwa umma, vivyo uendane na kuwapo utawala bora.

Rais Samia Suluhu Hassan, alipokutana na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, mnamo Februari 16 mwaka huu, jijini Brussels, Ubelgiji. PICHA: MTANDAO

Ndipo kutashuhudiwa utawala unaungwa mkono kwa kiasi kikubwa, pasipo kulazimishana. Ni mafanikio ambayo kwa kiasi kunahitaji dhana ya 'maridhiano' yanayochukua nafasi, hata kushuhudiwe umma kukubaliana.

Mara zote mtazamo na mustakabali wake, unarejea upepo wa siasa nchini kuhusu maridhiano yanayoendelea kufanyika kila kukicha. Mathalan, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Hassan Mwinyi anapoweka msimamo wake kukubaliana katika usimamizi wa kisiasa anaotumikia na kuwekwa kando kilichowafanya wavutane huko nyuma.

Itakumbukwa katika siku zake za mwanzo tu za siasa nchini, Rais Dk. Mwinyi akatamka anakosimamia kwamba "huu si wakati wa kufukua makaburi," akimaanisha kusahau misuguano iliyopita na kujikita pamoja kuijenga Zanzibar.

Hadi sasa kuna ushuhuda wa sura ya mafanikio makubwa kisiasa na nyendo za maendeleo, ikiwamo kinachojulikana sasa 'Uchumi wa Buluu' kujaza ngazi ya kinachofanyika kiuchumi katika sekta za utalii na kilimo cha karafuu visiwani na kamwe si msuguano.

**ANAKOPITA RAIS SAMIA**

Kwa Serikali ya Muungano, Rais Samia Suluhu Hassan, ametumia njia nyingi katika mantiki hiyo ya usuluhisho, akiamua mambo kadhaa ya kiutawala ngazi ya kitaifa na kukashuhudiwa mengi yakiridhiwa yenye sura ya umoja wa umma uliopo.

Msingi wake kimantiki, Rais Samia kwa kiasi kikubwa iko katika ambacho amekuwa akikitambulisha, pia matendo yake yana falsafa ya uongozi wa maneno kidogo, ila wenye maono, tafsiri na msimamo wa kina katika anachokifuatilia katika uongozi, sura ya pili nyuma ya pazia akiangalia mbali na hulka ya uzazi, katika yale anayotekeleza.

Ni katika staili hiyo ya uongozi hadi sasa kunashuhudiwa watuhumiwa wengi wa kisiasa wameachiwa huru kupitia kanuni ya kisheria ya serikali kutokuwa na haja ya kuendelea na baadhi ya kesi, ikiwamo uamuzi uliofanywa na serikali siku chache zilizopita.

Mara tu baada ya kufutiwa mashtaka mwaka huu na kutolewa rumande gerezani, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akakutana na Rais Samia na baada ya kipindi si kirefu akiwa na ujumbe wake, akakutana tena na Rais Samia, wakiambatana na wajumbe wa chama chake kujadiliana.

Ni uamuzi ulioshangaza wengi, lakini Mbowe akautetea kwamba ni fursa nyeti ambayo hakuwa tayari kuikosa, kwani ni ajenda yake ya muda mrefu, hata kabla ya kuingia jela .

Kisiasa, inaonekana kuwapo sura pana ya maridhiano kutoka chama hicho. Katika kikao chake cha uongozi kilichofanyika mjini Iringa, akaweka bayana ni nafasi aliyoitafuta sana wakati wote, kipindi ambacho CHADEMA imejiweka kando ikilalamikia mengi kisiasa.

Mbowe akakiambia kikao hicho cha wajumbe kinamaana kitaifa kwa chama chake, kwamba amefurahia kupata fursa ya kukutana na mkuu huyo wa nchi kujadili mustakabali wao, huku mwishoni mwa wiki iliyopita akifafanua sasa anaona nuru ya maridhiano kati ya chama chake na uongozi wa kiserikali.

Ni mustakabali ambao siku mbili kabla ya matamshi ya Mwenyekiti Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, ambaye sasa anaishi nje ya nchi, Ubelgiji, naye anakiri kuna ishara ya kutendewa haki na uongozi wa serikali madarakani.

Lissu, aliyekwishakuwa mbunge na mgombea urais kwa tiketi ya

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Juni 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580970

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Serikali yawaita kina Lissu, Lema

**YAJIBIWA** habari njema... *Endelea Ukurasa 2*



“Hakuna sababu yoyote kwa Mtanzania yeyote aliyepo popote pale ikiwamo viongozi wa CHADEMA waliopo nje ya nchi kutokurejea nchini.”

**Waziri Masauni**





Hivi karibuni Lissu akizungumza na Nipashe, alisema bado hajahakikishiwa usalama wake atakaporejea nyumbani kutokana na kuhofia watu wasiojulikana.

**Tundu Lissu**



“Ni kauli nzuri na nimefurahi kusikia kwani hakikisho la usalama sio tu lina faraja kwetu sisi tulio lazimika kukimbia, bali ni kwa watu wengi walio kuwa bado wana hofu.”

**Godbless Lema**

# Waziri ataja maeneo 10 yanayokula bajeti

UKURASA 4

# CCM yaungana na CUF, ACT kupinga tozo

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YATANGAZA SIKU KUTUA KOCHA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Asakwa tuhuma kumuua mkewe

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamsaka mwanamume anayedaiwa kumuua mke wake, Logesara Chitemo, mkazi wa Ukonga Mazizini jijini Dar es Salaam kwa kumchoma kwa kitu chenye ncha kali maeneo ya tumboni na kifuani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku na kwamba baada ya tukio hilo, mtuhumiwa alitoroka.

"Upelelezi wa tukio hili unaendelea na lazima akamatwe na atafikishwa kwenye vyombo vya sheria," Kamanda Muliro aliahidi.

Alisema mwanamke huyo enzi za uhai wake, alikuwa akifanya shughuli ya kuuza pombe ya kienyeji.

Akisimulia namna mauaji hayo yalivyotokea, Kamanda Muliro alisema kuwa wakati mwanamke huyo akiendelea na biashara hiyo, kuliibuka mzozo baina ya wawili hao.

"Mtuhumiwa (mume) alimshambulia (mke) kwa kitu chenye ncha kali na kumsababishia majeraha makubwa kifuani na tumboni, jitihada za kuokoa maisha ya mama huyu zilifanyika lakini baadaye alipoteza maisha," alisema.

Kumekuwa na idadi kubwa ya matukio ya wanandoa kuuana, sababu kubwa ikitajwa na viongozi wa vyombo vya usalama, wadau wa haki na sheria na viongozi wa dini kwamba ni wivu wa kimapenzi.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu dhamira ya benki hiyo kuendelea kutoa elimu ya fedha kupitia promosheni ya Mzigo Flexi ambapo inalenga kuwafikia Watanzania katika vitongoji vyote vya jiji hilo na nchi nzima, ili kutoa elimu ya mpango maalum wa kuweka akiba ambao utawawezesha kupata riba ya hadi asilimia 9. Kulia ni Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Benki hiyo, Badru Idd na (wapili kulia) ni Meneja wa Tawi la Azikiwe, Hamis Saleh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawaita kina Lissu, Lema

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imewataka Watanzania waliokimbia nchi kwa sababu mbalimbali wakiwamo viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kurejea nchini na kutumia fursa zilizoko kiuchumi kwa kuwa Tanzania ipo salama.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akitoa majibu kwenye swali la Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kuiagiza wizara hiyo kutoa majibu bungeni.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema hivi karibuni ameona Rais Samia Suluhu Hassan, akifanya mazungumzo na viongozi mbalimbali wa vyama vya upinzani kwa maana ya kuleta maridhiano na mshikamano wa nchi.

"Je, serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kueleza na kuwasihi Watanzania waliopo nje ya nchi ili waweze kurejea hapa nchini na kushiriki ujenzi wa nchi yetu," alihoji.

Hata hivyo, Spika Tulia kabla ya kumpa fursa Naibu Waziri wa wizara hiyo, Jumanne Sagini kujibu, alimtaka Sagini kutafuta majibu ya swali hilo ambalo ni la msingi na kuwa limekuwa likizungumzwa.

"Labda nikupe muda, jambo hili limeshazungumzwa zungumzwa sana, nikupe muda wa kuyatafuta hayo majibu utakapokuwa tayari utaniambia ili kabla ya kipindi cha maswali hakijaisha (jana) nitakupa fursa ya kujibu au kama hautakuwa nayo basi utakapokuwa tayari utaniambia kwa ajili ya kujibu swali hili ambalo limekuwa likizungumzwa zungumzwa," alisema Spika.

Baada ya kupitishwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/23, Spika Tulia alitoa nafasi kwa Waziri Masauni kutoa majibu hayo naye alisema nchi ipo salama na hakuna tishio lolote la usalama.

"Wimbi la ongezeko kubwa sana la wawekezaji wa Watanzania na wageni ni uthibitisho wa mazingira mazuri ya kiuchumi, kisiasa, kiusalama yaliyoko nchini, hivyo niwahakikishie Watanzania wote kuwa serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, itaendelea kuhakikisha hali ya kiusalama, kisiasa na kiuchumi iliyoko nchini inaendelea kudumu kwa maslahi mapana ya Watanzania wote," alisema.

Alisema Rais ameendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kiusalama nchini.

"Serikali itaendelea kusimamia vyombo vyake vya usalama kutekeleza majukumu yake ili haki isisemekane imetendeka bali ionekane kwa vitendo," alisisitiza.

Kwa upande wa kisiasa, alisema Rais Samia amefanya jitihada kubwa za kuimarisha mazingira hayo nchini ikiwamo kukutana na viongozi wa upinzani mara kadhaa.

"Mara zote hizo tumeshuhudia viongozi hao wakipongeza na kumsifia Rais hadharani kwa jitihada hizo, lakini ameshakutana na viongozi wa vyama vya siasa mmoja mmoja kwa mfano amekutana na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, baada ya kufutiwa mashtaka yaliyokuwa yakimkabili na pia amekutana na Tundu Lissu ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho nchini Ubelgiji baada ya Lissu kupeleka maombi hayo kwa Rais."

"Rais pia amekutana na Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo, Juma Duni, pia amekuwa akishiriki kwenye hafla mbalimbali za kijamii na kibinafsi zinazohusiana na viongozi wa vyama vya siasa mfano alishiriki kwenye uzinduzi wa Taasisi ya Maalim Seif Shariff Hamad, kule Zanzibar, majuzi alishiriki kwenye uzinduzi wa kitabu cha aliyekuwa Mbunge wa CHADEMA Sugu (Joseph Mbilinyi)."

"Mheshimiwa Rais mbali na kukutana na viongozi mmoja mmoja na kushiriki kwenye matukio yao, lakini amekutana na viongozi wa vyama kwa ujumla wake, pia amekutana na umoja wa vyama vya siasa vyenye uwakilishi bungeni ambapo walikuwa wakiongozwa na Zitto Kabwe kiongozi wa ACT-Wazalendo," alisema.

Kadhalika, alisema Rais Samia alishakutana na Baraza la Vyama vya Siasa na kilizaliwa kikosi kazi kinachoongozwa na Prof. Mukandala na kupitia Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi ilisababisha kuunda timu ya viongozi wa CCM na CHADEMA kushirikiana na kukabiliana na vikwazo vya kisiasa.

"Hakuna sababu yoyote kwa Mtanzania yeyote aliyepo popote pale ikiwamo viongozi wa CHADEMA waliopo nje ya nchi kutokurejea nchini, ili tu sio waweze kutumia fursa nyingi ambazo nimezieleza za maendeleo makubwa ya kiuchumi, kisiasa yaliyopo bali kushiriki kikamilifu kutoa michango yao kwa maendeleo ya nchi yao kwenye nyanja zote kwani hapa ni nyumbani kwao," alisema.

Hivi karibuni Lissu akizungumza na Nipashe, alisema bado hajahakikishiwa usalama wake atakaporejea nyumbani kutokana na kuhofia watu wasiojulikana.

Kuhusu hali ya kisiasa, alisema kuna ahueni kubwa na kwamba Rais Samia ameanza safari ya kuelekea kwenye mabadiliko.

**LEMA AFUNGUKA**

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini (CHADEMA), Godbless Lema, amesema kabla ya Krismasi mwaka huu, atakuwa amerejea nyumbani iwapo kauli ya kumhakikishia usalama wake iliyotolewa na serikali itatekelezwa kwa vitendo.

Nipashe ilitaka kujua lini atarejea nyumbani baada ya serikali kusema bungeni kuwa kwasasa wanahakikishiwa usalama wao wanaweza kurejea nyumbani, kwa kuwa vyombo vya ulinzi na usalama viko macho na hakuna matukio yaliyowafanya wakimbie nchi.

Lema ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini na Mjumbe wa Kamati Kuu, alisema:

"Ni kauli nzuri na nimefurahi kusikia kwani hakikisho la usalama sio tu lina faraja kwetu sisi tulio lazimika kukimbia, bali ni kwa watu wengi walio kuwa bado wana hofu," alisema.

"Amani na haki vinajenga furaha na taifa lenye furaha ni taifa lenye mafanikio. Hofu ya mtu mmoja juu ya uhai wake isipuuzwe hata kidogo kwani kukimbia nchi ni maisha ya huzuni sana na ni 'experience' (uzoefu) mbaya."

Alisema hakuna huzuni kubwa katika maisha kama kutembea huku unatazama nyuma kuangalia kama unafuatwa na mtu akuibie kama kibaka anavyopora simu au akuponde kichwa kama nyoka.

"Kwa hiyo kauli yoyote inayo ashiria amani kwa mtu mmoja ni inayojenga furaha kwa nchi nzima. Nitahifadhi taarifa hii kwa ajili ya watoto wangu ili wajue kuwa sikuwa 'criminal' (mhalifu) kukimbia nchi," alifafanua Lema.

"Lakini faraja zaidi ni kuwa pengine vikao vya maridhiano kati ya CHADEMA na serikali vinaanza kuwa na mwelekeo mzuri. Matumaini yangu kuwa wema mwingi utazaliwa katika hoja muhimu zilizoko mezani."

"Ninajua ndugu zangu wanafuatilia sana habari za Bunge, nina amini wakiona kesho (leo) katika magazeti watafurahi na kupata amani. Mama yangu atasema moyoni mwake, Godbless wangu Krismasi hii nitakuwa naye," alisema na kuongeza:

"Nimalizie kwa kusema kuwa kuna siku isiyo na tarehe kila yaliyofanyika gizani yataonekana hadharani kwani haki ni vita ya Mungu. I will be home soon now (nitakuwepo nyumbani karibuni) nikiamini maneno yenye vitendo ni faraja kwa kila mtu," alisema.

# Sabaya kufanyiwa upasuaji wa nundu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

IDADI ya washtakiwa katika kesi mpya ya uhujumu uchumi na rushwa inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, imeongezeka na kufikia watano huku mahakama hiyo ikielezwa kuwa Sabaya anatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa nundu kichwani.

Aliyeongezwa katika kesi hiyo kutoka washtakiwa wanne hadi kufikia watano, ni mfanyabiashara Antero Assey (43), Mkazi wa Moshi mkoani Kilimanjaro.

Assey alipofikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Salome Mshasha anayesikiliza shauri hilo, alisomewa mashtaka na Wakili wa Serikali Mwanandamizi Verdiana Mlenza, aliyedai mshtakiwa huyo wa tano anakabiliwa na kosa la kuongoza genge la uhalifu katika Wilaya ya Hai Februari 2, mwaka jana.

Mashtaka mengine aliyosomewa ni pamoja na la pili ambalo linamkabili mshtakiwa wa kwanza, Sabaya ambapo anadaiwa kulifanya Februari 22, mwaka jana kwa kuomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomangombe, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Katika shtaka la tatu, Ole Sabaya peke yake, anadaiwa kujipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai kwa nia ya kuzuia taarifa za uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi.

Wakati shtaka la nne na la tano linawakabili mshtakiwa wa pili, tatu, nne na tano, ambalo ni kumsaidia mshtakiwa wa kwanza (Ole Sabaya), kushawishi na kujipatia manufaa asiyostahili ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Alex Swai, huku akijua ni kinyume cha sheria.

Katika shtaka la sita linalomkabili mshtakiwa wa kwanza (Sabaya) ni la madai ya ukiukwaji wa maadili ya utumishi, akiwa ni mtumishi wa umma katika Wilaya ya Hai na shtaka la saba ni utakatishaji wa fedha ambalo linawakabili washtakiwa wote.

Upande wa utetezi katika kesi unaongozwa na Wakili Helena Makunda, akisaidiwa na Wakili Hekima Mwasipu.

### UPASUAJI NUNDU KICHWANI

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Wakili wa Utetezi, Helena Makunda, alisimama na kuiomba Jamhuri kuhakikisha inakamilisha upelelezi mapema kwa kuwa mshtakiwa wa kwanza, Sabaya ni mgonjwa.

"Mheshimiwa Hakimu, mshtakiwa wa kwanza ni mgonjwa na anatarajia kwenda kufanyiwa operesheni ya nundu ya kichwa kutokana na kupata ajali akiwa kazini.

"Tunaiomba mahakama yako tukufu, kuangalia uwezekano wa kukamilisha taratibu zake kwa wakati ili kesi hii ianze kusikilizwa na kila mshtakiwa ajue hatima yake.

"Mwanzoni Jamhuri ilisema ushahidi umekamilika, leo (jana) wanasema ushahidi haujakamilika. Tunashindwa kuelewa," wakili huyo alidai.

Baada ya pande zote kutoa hoja zao, Hakimu Mshasha aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 20 mwaka huu itakapotajwa tena mahakamani huko.

### NJE YA MAHAKAMA

Kabla ya kutajwa kwa kesi hiyo inayovuta hisia za Watanzania wengi, baadhi ya wananchi, waliingia katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi wakiwa wamebeba majani aina ya masale, ambayo hutumiwa na kabila la Wachaga kuombana msamaha.

Kwa jamii ya huko, masale kwa Wachaga ni moja ya majani yanayoheshimika kwenye mila zao kwa kuwa hutumika kuomba msamaha.

Majani hayo pia hutumika kuwapatanisha watu walio katika mgogoro na endapo mmoja atakosea na kuomba msamaha kwa kutumia majani hayo, inaaminika kimila kwamba hakuna sababu ya kutoukubali msamaha huo.

## CCM yaungana na ACT, CUF kupinga tozo Zenji

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

VYAMA vitatu vya siasa vimepinga mabadiliko ya tozo ya usafi yaliyofanywa na Kampuni ya Vigors Clean inayomilikiwa na Mfanyabiashara Toufky Salum Turky na kutumika katika Jiji la Zanzibar kuanzia Julai, mwaka huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari, viongozi waandamizi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Wananchi CUF na Chama cha ACT- Wazalendo, wamesema mabadiliko ya tozo hizo yana madhara makubwa kwa maendeleo ya sekta ya biashara na utalii.

"Kupandisha tozo ya usafi katika migahawa na maduka kutoka Sh. 50,000 mpaka 500,000 kwa mwezi kuna madhara makubwa kwa maendeleo ya sekta ya biashara na utalii Zanziba," alisema Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Catelina Peter Nao.

Alisema kabla ya mabadiliko hayo, Kampuni ya Vigors Clean, ilitakiwa kukaa pamoja na wadau na Baraza la Manispaa Wilaya ya mjini badala ya kupandisha ghafla na kusababisha mtafaruku mkubwa kwa wafanyabiashara na wawekezaji sekta ya utalii.

Catelina alisema Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekuwa akisisitiza umuhimu wa kuwapo kwa unafuu wa tozo za ada kwa wafanyabiashara na wajasiriamali ili kuharakisha maendeleo ya sekta ya biashara visiwani humo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uenezi na Habari wa ACT-Wazalendo, Salum Diman Abdalla, alisema serikali inapaswa kuingilia kati ili kunusuru sekta ya biashara na utalii visiwani hapo.

Alisema kabla ya kufanyika mabadiliko ya tozo za usafi kampuni hiyo ilitakiwa kufanya utafiti badala ya kupandisha ghafla bila ya kujali maslahi ya taifa na maendeleo ya sekta ya biashara na utalii.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Mbarouk Seif, alisema kama mabadiliko ya tozo mpya yatatekelezwa, migahawa mingi italazimika kufungwa na watu kupoteza ajira.

Seif alisema serikali inapaswa kutoa msimamo kabla ya malipo ya tozo mpya ya usafi kuanza kutumika Julai mwaka huu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji katika Sekta ya Utalii Zanzibar, Rahim Bhaloo ameponpeza hatua ya Baraza la Manispaa Wilaya ya Mjini ya kupinga mabadiliko ya tozo yaliyofanywa na Kampuni hiyo.

"Wakati umefika kwa baraza la manispaa mjini na Kampuni ya Vigors Clean kukaa pamoja kupitia upya tozo mpya za usafi ili kuleta unafuu kwa maendeleo ya sekta ya utalii na biashara.

Aidha, aliwataka wamiliki wa hoteli na migahawa kujiunga na jumuiya ya wawekezaji katika sekta ya utalii ili kuwa na sauti ya pamoja katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza sekta ya utalii na biashara.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
07.06.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Ijumaa tarehe **10-06-2022 hadi 14-06-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd / Raphael Logistics Ltd** zitasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **JNHPP SITE,** gari hizo zenye namba za usajili:
**KBQ 623 Z / ZD 9920 T 204 DYJ / T 232 ABE**
**T 133 CCP / T 232 ABE T 602 DPQ / T 190 DHG T 441 DXU / T 724 DNM**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23**
**Upana - mita 7.40**
**Kimo - mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: **BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia KILWA ROAD, KIBITI, MLOKA.**

Gari litasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka Dar es Salaam Port mpaka Bungu.

Kutoka Bungu kwenda JNHPP Site gari litasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

116890702



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
06 - 06 - 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe **09 – 06 – 2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zenye namba za usajili:
**T 622 DFA / T 777 AQR T 645 DFA / T 310 DDH T 653 DFA /T 416 AYQ**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 20**
**Upana - mita 4.30**
**Kimo - mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

116890702



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
06 - 06 - 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Alhamisi tarehe **09 – 06 – 2022** kampuni ya Mainline Carriers Ltd. itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zenye namba za usajili:
**T 468 DYG / T 837 DJB T 464 DYG / T 887 DJB T 203 DJY / T 837 DJB**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 22**
**Upana - mita 4.60**
**Kimo - mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

116890702

# Waziri ataja maeneo 10 yanayokula bajeti

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ametaja maeneo 10 yaliyotafuna asilimia 82.5 ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha unaoisha mwezi huu, akisema matumizi yake hayakwepeki.

Dk. Nchemba alifafanua jana bungeni wakati akihitimisha hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, kwamba kati ya Sh. trilioni 19.99 zilizotengwa kwa matumizi ya serikali kwa mwaka huo, Sh. trilioni 16.5 zilielekezwa kwenye maeneo hayo.

"Hapa unaongelea mahitaji usiyoweza kuyaahirisha ambayo ni Sh. trilioni 16.5 kati ya Sh. trilioni 19.99 ambayo fedha zimehifadhiwa mahususi kwa matumizi hayo," alisema.

Waziri aliyataja maeneo hayo ni: Deni la Taifa; miradi ya barabara; maji; Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo; mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; umeme vijijini (REA); mishahara ya watumishi wa umma; afya; hifadhi ya jamii; na uwekezaji katika reli.

Kwa mujibu wa Dk. Nchemba, mchanganuo wake ni: Deni la Taifa Sh. trilioni 6.9; mishahara Sh. trilioni 6; miradi mikubwa ya reli Sh. trilioni 1.45; mikopo ya elimu ya juu Sh. bilioni 423.5, Umeme Vijijini (REA) Sh. bilioni 367; maji Sh. bilioni 346; na elimu bure Sh. bilioni 202.

Kuhusu miradi ya barabara, alisema Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Sh. bilioni 579; Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Sh. bilioni 414.

Alisema Afya inachukua Sh. trilioni 2.5; Elimu Sh. trilioni 5.6; Maji Sh. bilioni 800.5; na Hifadhi ya Jamii Sh. trilioni 1.8.

Waziri alisema makusanyo ya ndani yalikuwa Sh. trilioni 9.99, ambayo katika uhalisia ni pungufu kwa Sh. trilioni 10 dhidi ya matumizi halisi ya bajeti ya serikali aliyoyataja.

"Haya ni matumizi mengine huwezi kurudi nyuma, pawe na UVIKO-19, vita Ukraine na ukame, haya ni matumizi huwezi kuyaahirisha.

"Kazi hii ndiyo inamfanya Rais Samia Suluhu Hassan asilale, ndiyo maana unaona leo yuko huku yuko kule. Na wengine wanadhani haya mambo yanaweza kwenda hata pasipokuwa na jua limewaka," alifafanua.

Waziri Nchemba alitumia fursa hiyo bungeni, kuwaelimisha wajumbe mzigo ulio mbele ya Mkuu wa Nchi, Rais Samia na jitihada anazotumia kukabiliana nao, ikiwamo kuonana na Makamu wa Rais wa Marekani, alipotamka:

"Niwaulize swali dogo tu, ni waziri gani wa nchi za Afrika anaweza kutafuta kuonana na Rais wa Benki ya Dunia (WB) ndani ya wiki moja au ndani ya siku tatu, akaonana na Rais wa Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF)?

"Haya ni mambo ambayo yanafanyika kwa uzito wake, Rais anaona ayaongezee nguvu na ndiyo maana alipokwenda nchi za Ulaya, alionana na taasisi zote za maendeleo."

Waziri huyo, Mbunge wa Iramba na kitaaluma ni mchumi, alieleza kwamba mikoa yote imepata fedha za miradi ya maendeleo, akisifu inatekelezwa kwa ufanisi.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kamati: Taasisi za serikali ziache kufanya biashara

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Bajeti imetoa mapendekezo sita kwa Wizara ya Fedha na Mipango ikiwamo kutenga fungu maalum kwa ajili ya Deni la Serikali, kubadili sheria ya ununuzi, mashirika ya umma kuacha kutoza fedha badala ya kutoa huduma na kutekeleza miradi kwa kushirikisha sekta binafsi.

Akiwasilisha bungeni jana maoni ya kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, Makamu Mwenyekiti wake, Omari Kigua, alisema wanaipongeza serikali kwa kukubali kuanzisha fungu jipya litakalokuwa linahusika na ulipaji wa Deni la Serikali tu.

"Hatua hii itaondoa mkanganyiko uliokuwapo wa kujumlisha madeni ya serikali na huduma za mfuko wa serikali," alisema.

**MIRADI SEKTA BINAFSI**

Kigua alisema kamati ilibani njia nzuri na rahisi ya kujenga miundombinu ya mawasiliano, huduma, usafiri na usafirishaji ni kwa kutumia ubia baina ya sekta ya umma na binafsi.

Alisema pamoja na uwapo wa sheria tangu mwaka 2010, njia hiyo haijaweza kulinufaisha taifa kwa zaidi ya miaka 12 sasa na mara kadhaa kamati imeshauri serikali kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ubia, ili kupunguza kiwango cha mtaji kutoka dola za Marekani milioni 20 hadi walau kati ya dola milioni mbili hadi milioni tano kwa Watanzania na kwa wageni kati ya dola milioni tano hadi milioni 10.

"Hatua hii si tu itavutia wawekezaji kutoka nje bali watanzania watakaweza kushiriki kwenye ujenzi na utoaji wa huduma kwa mfumo wa ubia," alisema.

**MABADILIKO YA KODI**

Mwenyekiti huyo pia alisema kikosi kazi cha mabadiliko ya kodi kilianzishwa ila hakijatoa mrejesho kwa wadau mbalimbali waliofika mbele yake, ili kuwajulisha ni kwanini mapendekezo yao hayajakubaliwa.

"Hali hii husababisha masuala yanayowasilishwa katika kikosi kazi kujirudia kila mwaka na hayafanyiwi kazi. Kamati inaishauri serikali kuweka utaratibu wa kutoa mrejesho kwa wadau waliofika mbele yake, ili hoja zinazowasilishwa zisijirudie mara kwa mara bila majibu," alisisitiza.

Alisema kamati ilipendekeza kuangalia muundo wa wajumbe wa kikosi kazi hicho na itolewe fursa ya kualika wataalamu wengine pale inapobidi.

**NIDA**

Kigua pia alisema maduhuli kwa baadhi ya maeneo yanaondoa hamasa ya kutoa huduma na badala yake wizara, idara, au mamlaka za serikali hasa ambazo hazifanyi biashara zinaanzisha au kutoza viwango vikubwa vya ada na tozo, ili kukusanya maduhuli na kusahau kwamba jukumu lao la kwanza ni kutoa huduma.

Alitoa mfano wa taasisi hizo ni taasisi yoyote inapotaka kupata taarifa za mtu kwa matumizi ya rasmi kutoka NIDA zinatozwa Sh. 500 kwa kila taarifa anayoitaka muhusika.

"Hivyo, ni wazi kwamba kazi inayofanywa na NIDA ya kusajili Watanzania wote, ili watambulike imegeuka kuwa biashara na si huduma tena," alisema.

**SHERIA YA UNUNUZI**

Makamu Mwenyekiti huyo alisema ni muhimu wa kubadilisha Sheria ya Ununuzi wa Umma, ili iendane na wakati kutanzua kero mbalimbali ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wake.

Alizitaja baadhi ya kero kuwa ni matumizi ya sheria hiyo kwa mashirika na taasisi za umma ambazo zinajiendesha kibiashara imekuwa na shida, mfano TTCL haiwezi kununua minara ambayo imetumika.

"Inachelewesha mchakato wa ununuzi katika mashirika ya umma yanayojindesha kibiashara, ambayo uamuzi wa haraka unatakiwa kufanyika ili biashara iendelee.

"Kamati inaishauri serikali kubadilisha sheria hiyo ili iendane na mahitaji ya sasa," alisema.

## Wizara yamulika maeneo manane

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 itaweka kipaumbele kwenye maeneo manane ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Akiwasilisha bungeni jijini hapo jana makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23, Waziri wake, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema wanatarajia kutekeleza kwa kuzingatia malengo, shabaha na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati.

Aidha, vimezingatia malengo, shabaha na vipaumbele vya mpango na bajeti ya mwaka 2022/23 vimeibuliwa kutoka kwenye Mpango Mkakati wa Wizara 2021/22 - 2025/26, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 na Ilani ya CCM.

Dk. Nchemba alivitaja vipaumbele hivyo ni kukusanya, kutafuta na kudhibiti mapato na matumizi ya serikali, kuhudumia kwa wakati deni la serikali pindi linapoiva.

Pia kufanya tathmini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ikiwa ni maandalizi mahsusi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Alisema kingine ni kufanya tathmini ya mfumo na muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili kuwezesha kutungwa kwa sera ya taifa ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

Dk. Nchemba alisema kipaumbele kingine ni kurejesha Bahati Nasibu ya Taifa, kufanya utafiti katika sekta za uzalishaji ili kuibua fursa za uwekezaji, uwezeshaji na vyanzo vya mapato ya serikali katika muda mfupi, kati na mrefu.

Pia kuendelea kutekeleza maagizo ya serikali ya kutafsiri sheria za wizara na taasisi zake kwa lugha ya Kiswahili na kuhuisha mwongozo wa Taifa wa usimamizi wa viashiria hatarishi.

Waziri huyo alisema upande wa matumizi ya maendeleo, wanatarajia kujielekeza kwenye kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma kupitia programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma awamu ya sita (PFMRP VI).

Pia, kuandaa na kujenga ghala la takwimu, kuratibu na kusimamia zoezi la Sensa ya Watu na Makazi, kuziwezesha taasisi za wizara, hususan taasisi za elimu na mafunzo kuboresha miundombinu ya kujifunza na kufundishia.

Vilevile, kuendelea na ujenzi wa jengo la wizara katika Mji wa Magufuli, Mtumba Dodoma, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mhakikimali na Hazina Ndogo katika mkoa wa Geita, Njombe na Songwe.

Eneo lingine ni ukarabati wa jengo la wizara lililoko jijini Dar es Salaam, Hazina Ndogo Morogoro, Kigoma na Ruvuma.

Kwa upande wa vipaumbele vya taasisi, alisema: "Wizara inatekeleza baadhi ya majukumu yake kupitia taasisi za elimu na mafunzo na elimu ya juu, bodi za kitaalamu na kitaaluma, usimamizi wa fedha, kodi, bima, ununuzi na ugavi, michezo ya kubahatisha, uwekezaji na uwezeshaji pamoja na takwimu."

Bunge liliidhinisha jana makadirio ya mapato na matumizi ya Sh. trilioni 14.94 kwa ajili ya wizara hiyo. Kati yake, Sh. trilioni 13.62 matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 1.32 za matumizi ya maendeleo.

HABARI KITAIFA

# Aliyekuwa kigogo wa CWT ajitetea fedha safari ughaibuni

**Na Grace Gurisha**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif (46), amedai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa alikwenda kuangalia mpira wa miguu mchini Cape Verde kwa fedha zake binafsi na sio za chama hicho kama inavyodaiwa.

Seif alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate, wakati akitoa utetezi dhidi ya kesi ya matumizi mabaya ya madaraka na kuchepusha fedha Sh. milioni 13.9 mali ya CWT.

Alidai kuwa, alikwenda kuangalia mpira wa miguu nchini Cape Verde wakati Taifa Stars ilipokuwa kwenye mashindano ya AFCON, Oktoba 10, 2018 na kurudi nchini Oktoba 13, 2018 kutokana na hamasa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) pamoja na serikali.

Pia, alidai safari ya kwenda huko iliratibiwa na TFF, lakini kwa upande wake nauli pamoja na malazi aligharamia mwenyewe kwa sababu alikuwa ana fedha za kutosha kutokana na mshahara wake na posho za vikao.

"Safari ilitokana na mshahara wangu, posho za vikao kama kwenda Cape Verde ni Sh milioni 3.3 kwa nafasi yangu nisingeweza kushindwa kulipia kwa sababu pia mimi nilikuwa mjumbe wa TFF kwa hiyo nilikuwa na fedha," alidai Seif.

Kadhalika, alidai kabla ya kwenda Cape Verde alikuwa ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu, Mkoa wa Geita na pia alikuwa mjumbe wa mkutano Mkuu wa TFF, asingeshindwa kusafiri kwa fedha yake.

Kuhusu tuhuma za kukata fedha za Mkuu wa Idara ya Jinsia na Wanawake wa CWT, Stella Mamoto, ambaye alikuwa anakwenda kushiriki mafunzo nchini Japan, alidai kuwa Mamoto alisafiri vizuri na aliporudi alikwenda kuripoti CWT. Hata hivyo, Seif alikataa tuhuma za kuchepusha fedha hizo na kutumia madaraka yake vibaya kwa kuwa yeye anafanya kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu za chama hicho.

Akiongozwa na Wakili wake, Nestory Mkoba, alidai kuwa kuna shahidi wa upande wa mashtaka Prosper Lubuva, ambaye ni Mkurugenzi Elimu na Mafunzo wa CWT na kudai mahakamani kuwa alikata fedha za Mamoto.

Seif, aliendelea kudai kuwa hajawahi kufanya hivyo na alipoulizwa kama ana ugomvi na Lubuva alidai alishawahi kumuandikia barua ajieleze kutokana na utendaji kazi wake na alipomrudishia majibu hayakumridhisha na kupeleka suala lake mbele.

"Majibu yalivyotoka Lubuva alihamishwa kikazi kwenda Wilaya ya Bukoba kuwa Katibu wa CWT katika wilaya hiyo, kwa hiyo inawezekana ana chuki na mimi, lakini mimi sina chuki naye kwa sababu pia alishawahi kunifungulia kesi CMA."

Awali, Seif na Mwekahazina wa chama hicho, Abubakari Allawi, wanaokabiliwa na mashtaka ya kutumia madaraka yao vibaya, walidai mahakamani hapo kuwa wanatarajia kuwa na mashahidi wanane na vielelelzo.

Washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Oktoba 3, 2018 na Novemba 6, 2018, katika ofisi za CWT zilizopo Kinondoni, wakiwa waajiriwa wa chama hicho, walitumia mamlaka yao vibaya kwa kujipatia Sh. 13,930,693.

Katika Shtaka la pili, siku na maeneo hayo, Seif na Allawi, kwa kutumia madaraka yao vibaya na kwa manufaa yao wenyewe wanadaiwa kuchepusha fedha Sh. milioni 13.9 mali ya CWT.

Viongozi hao wanadaiwa kutumia fedha hizo kwa ajili ya safari ya kwenda Cape Verde, kuangalia mpira wa miguu.

## Bil. 78/- kuongeza upatikanaji mafuta na sukari nchini

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema Benki ya Maendeleo ya Kilimo imepanga kutoa mikopo ya takriban Sh. bilioni 78 kwa sekta ya viwanda, hususan viwanda vya mafuta ya kula na sukari katika mikoa ya Kigoma, Shinyanga na Manyara kwa mwaka 2022/23.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Nchemba alisema mikopo hiyo inatarajiwa kupunguza upungufu wa mafuta ya kula na sukari nchini.

"Benki hiyo pia imepanga kutoa mkopo wa takriban Sh. bilioni 130 kwa ajili ya ununuzi wa pamba na kahawa,"alisema.

Pia alisema Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) imepanga kutoa mikopo ya takriban Sh. bilioni 47 kwa sekta za viwanda, maji, nishati, madini, mafuta na gesi, huduma na utalii pamoja na kilimo ili kukuza mizania ya benki kufikia Sh. billioni 902.63.

Alisema lengo ni kupunguza ukwasi kwa kuongeza mtaji wa benki kwa Sh. bilioni 373; na kuuza hati fungani zenye thamani ya Sh. bilioni 300.

Alisema Benki ya Biashara Tanzania (TCB) imepanga pamoja na mambo mengine, kuboresha uwezo wa benki wa kuzalisha mapato, ili kufikia Sh. bilioni 185.6; kukuza faida ya benki kabla ya kodi ili kufikia Sh. bilioni 21.4; kutoa mikopo salama ya Sh. bilioni 709.

Pia watakusanya amana za wateja Sh. bilioni 974; kukuza mali za benki ili kufikia Sh. bilioni 1,257; na kukuza thamani ya hisa na kufikia Sh. bilioni 128.


VETA | equinor

# TANGAZO

## Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) – Lindi

### Ufadhili wa masomo –Ngazi ya Tatu unaotolewa na Equinor na Shell - 2022/2023.

**Makao Makuu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)** kwa niaba ya VETA – Lindi kwa kushirikiana na ***Equinor Tanzania AS na Shell Exploration and Production Tanzania Ltd,*** zinachukua nafasi hii kuwakaribisha wanafunzi wanaotaka kuchukua mafunzo ya ufundi Stadi Daraja la 3 (VC III), katika fani sita zinazotolewa katika Chuo cha VETA Lindi ambazo ni Ufundi Magari(MVM), Uashi(MB), Viyoyozi na Majokofu(RAC), Umeme(EL), Ubunifu wa Mavazi, Ushonaji na Teknolojia ya Nguo(DSCT), Uchomeaji na Uungaji Vyuma(WF)

Ufadhili huu utagharimia ada, bima ya afya, malazi, chakula, usafiri na kutoa vitendea kazi vya kuanzia mara baada ya kumaliza na kufaulu mafunzo hayo. Ufadhili huu ni wa miezi 12.

**Vigezo**

- Mwanafunzi ni lazima awe amemaliza na kufaulu mafunzo ya Daraja la II, ili aweze kufirkiriwa kujiunga na mafunzo ya Daraja la III.
- Mwanafunzi ni lazima awe amefaulu Kidato cha Nne na awe na cheti.
- Ufadhili huu unatolewa kwa vijana wa Mkoa wa Lindi tu aidha awe mkazi au mzawa mwenye umri usiozidi miaka 35.
- Wanafunzi wakike, wenye mahitaji maalumu (ulemavu), wanaotoka katika familia za kipato cha chini watapewa kipaumbele na ambao hawapata ajira rasmi kipaumbele

**Taratibu za kuomba**

Muombaji atatakiwa kufuata taratibu zifuatazo wakati wa kutuma maombi:

- Kutuma barua ya maombi akiambatisha Cheti cha Kidato cha Nne na cha Daraja la II cha Ufundi Stadi (VC II) au Taarifa ya matokeo kutoka Ofisi ya Kanda.
- Kulipia Shilingi 5000 ambazo hazitarudishwa kwa kupitia Control No, ambayo ataichukuwa katika ofisi za VETA -Lindi.
- Kutuma maombi yake kwa njia ya kielektronia au kwa barua kwa kutumia anuani iliyotolewa katika tangazo.
- Kuambatanisha barua inayomtambulisha na kuthibitisha kuwa muombaji ni makazi au mzawa wa Lindi kutoka Serikali ya Mtaa/Kijiji.

**Tarehe ya mwisho wa maombi ya ufadhili**

Mwisho wa kutuma maombi VETA Lindi ni tarehe 30/6/2022. Usahili utafanyika kwa wanafunzi ambao watakuwa wamechaguliwa kujiunga na masomo na kupewa barua ya kujiunga na chuo kusoma Ngazi ya III katika fani zilizotajwa hapo juu. Na Programu itaanza mwezi Julai 2022.

**Kwa mawasiliano**

**Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi – VETA**
**S.L.P 1001 Lindi**
**Tel: +2555232935150/0718211638**
**Baruapepe: lindirvtsc@veta.go.tz**

***Wanawake na walemevu wanatakiwa kujitokeza zaidi kuomba ufadhili huu***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusimwangushe Rais miradi ya maji

**JUZI** Rais Samia Suluhu Hassan, alishuhudia utiaji saini mikataba ya miradi ya maji kwa ajili ya miji 28 ya Tanzania Bara itakayogharimu Shilingi trilioni 1.7.

Hii ni hatua muhimu kwa nchi yetu ambayo katika baadhi ya maeneo yanakabiliwa na uhaba mkubwa wa majisafi na salama kwa wananchi wake.

Utiaji saini huo ulifanyika jijini Dodoma na Rais Samia alitoa angalizo kwa fedha hizo kutumika vizuri kwa kuwa ni mkopo utakaolipwa na Watanzania wote.

Juhudi za Rais Samia kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma muhimu zinaonekana na Watanzania wana kila sababu ya kumuunga mkono kwa kutomuangusha inapokuja kwenye suala la utekelezaji.

Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa kwa ushirikiano wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF), mabilioni ya watu duniani wanaendelea kutaabika kutokana na kukosa huduma bora za maji na masuala ya usafi.

Hivyo, suala la upatikanaji majisafi na salama linahusu watu wote kuanzia mijini hadi vijijini na mkopo huo ilioupata Tanzania katika kutekeleza miradi mipya ya maji ni muhimu katika kuwaondoa Watanzania kwenye ukosefu wa huduma hiyo na hatimaye waweze kunufaika nayo.

Wakati wa utiaji saini Rais Samia, aliwatahadharisha makandarasi kutozidisha faida kwa lengo la kuiumiza serikali na kupata hasara.

Pia, ni vizuri kuzingatia kuwa fedha hizo ni mkopo na kila Mtanzania ataulipa, hivyo hasara itabebwa na wote wakiwamo hao wakandarasi watakaopewa kazi hiyo kwa utekelezaji.

Lengo la serikali ni kuona majisafi na salama yanapatikana kwa asilimia 85 vijijini na baadhi ya vyanzo vinavyotegemewa katika miradi hiyo ni Ziwa Victoria.

Waziri wa Maji, Juma Aweso, amemhakikishia Rais kusimamia miradi hiyo na kukamilika kama inavyotarajiwa, ili kuwanusuru wananchi hasa kinamama na athari zinazotokana na uhaba wa maji.

Baadhi ya miji itakayonufaika katika mradi huo imetajiwa kuwa ni Handeni, Korogwe, Pangani, Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Chunya, Rujewa, Wanging'ombe, Makambako, Njombe, Kiomboi, Singida, Manyoni, Chemba na Chamwino.

Miji mingine ni Kasulu, Mpanga, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Geita, Chato, Mafinga, Newala, Tandahimba, Nanyamba, Rorya na Songea.

Inaelezwa kuwa ndani ya mwaka mmoja miradi ya maji katika Wizara ya Maji imetekelezwa kwa asilimia 90, huku bajeti ya maji kwa mwaka huu wa fedha ikiwa tayari imeshapitishwa.

Ripoti ya UN ya mpango wa ufuatiliaji wa "hatua kuhusu maji ya kunywa na masuala ya usafi :2000-2017, ikilenga kutokomeza usawa, imebaini kwamba wakati kuna hatua kubwa zilizopigwa katika kufikia fursa ya msingi ya maji kwa wote, usafi na huduma za majisafi, bado kuna pengo kubwa katika ubora wa huduma zinazotolewa katika masuala hayo.

Umuhimu wa huduma ya maji kwa binadamu ni mkubwa na maji ni uhai, bila huduma hiyo hakuna kitakachoendelea.

Kama alivyotahadharisha Rais Samia kuhusu usimamizi wa miradi hiyo ya maji, ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha hakuna kitakachoharibika ni kwa faida ya wote bila kujali kabila, dini, rangi, mtoto, mzee, maskini au tajiri.

Pamoja tukijitoa kulinda na kusimamia miradi hiyo wananchi watakombolewa na adha ya ukosefu wa huduma hiyo muhimu na kufurahia maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Haule

# Ulinzi wa mazingira uwe ajenda namba moja

**WATANZANIA** wanalazimika kutumbua wajibu wao wa kutunza na kuyahifadhi mazingira na kuachana na fikra kuwa ni jukumu la serikali na viongozi pekee yao. Wafahamu kuwa ni kazi ya wote ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayomtikisa kila mmoja.

Wadau wa mazingira wanapozungumza na Nipashe kuhusu uhifadhi wa mazingira wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani iliyofanyika Jumapili Juni 5, wanasema lazima watu waamke na wajitambue ili kutekeleza wajibu huo.

Balozi wa Mazingira ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Chage Alex, anakumbusha kuwa ni muhimu kuhifadhi mazingira kutokana na kitisho cha mabadiliko makubwa ya tabianchi.

Ni wazi kuwa siyo kificho watu wameshuhudia athari za mabadiliko ya tabianchi kama maji kupungua katika mito na mabwawa kukauka. Mfano ni Mto Ruvu na Bwawa la Mindu yote hayo si mapya kwa Watanzania hasa wakazi wa Dar es Salaam pamoja na Pwani na Morogoro wameshuhudia uhaba wa maji.

Uharibifu wa mazingira unapunguza maji ambayo ni kila kitu katika maisha ya mwanadamu na yamekuwa tegemeo kubwa kwenye uzalishaji malighafi viwandani na ni kitu muhimu kwa uchumi wa nchi kuanzia shambani, nyumbani, hospitalini, vyuoni, shuleni hadi viwandani.

Uchumi wa nchi unategemea maji, chakula pia kinategemea maji, ndiyo unaofua umeme, unaotumika viwandani na nyumbani, ujenzi unayategemea na vitu vyote hivyo ni muhimu jukumu kubwa likibakia kulinda maji na vyanzo vyake.

Aidha, maji yakikosekana umeme unasumbua ukikosekana uzalishaji unayumba na kuyumbisha uchumi utakaoshuka na hakuna atakayekuwa na muda wakusikiliza siasa wala habari za vyama ikiwa uchumi unayumba na kukwamisha maendeleo, hivyo ulinzi wa mazingira ni kuanzia sasa uwe ajenda namba moja.

Ni wajibu wa serikali zote kuu na mitaa kuendelea kuipa kipaumbele agenda ya mazingira kwa sababu ni mhimili wa unaotegemewa na watu, mifugo, kilimo na umeme na kwamba hivi karibuni zipo sehemu wafugaji wamelia kwa kupoteza mifugo kwa sababu ya ukame.

Juhudi ziende pamoja na kutoa elimu kwa umma kuwachukulia hatua wanaofanya uchafuzi wa mazingira hasa wanaoendesha kilimo kando ya maji, kulisha mifugo chini ya madaraja kwani kwa kuwapa elimu maeneo hayo yatakuwa salama zaidi kwa sababu ndiyo wakazi na walinzi wa rasilimali kuanzia maji, misitu na uoto wa asili.

> **Kwa kauli yake jamii inapaswa kuelewa na kuzingatia utekelezaji wa sheria za mazingira zilizoko kwa sababu licha ya kuwa na sheria bora lakini utekelezaji na usimamizi wake umekuwa tatizo na hauonekani.**

Aidha, wadau wa mazingira kama viwanda vya maji au juisi wanapaswa kujua kuwa wana jukumu zito la kuhifadhi mazingira kwa sababu chupa za plastiki zinazotokana na bidhaa zao ni nyingi tena zinazagaa mitaani hivyo ni lazima wakae na serikali ili kuona namna watakavyochangia kudhibiti uchafuzi huo.

Kama ambavyo mratibu wa kikundi kazi cha misitu Tanzania (TFWG) Casian Sianga, anavyosisitiza kuwa kuhifadhi mazingira na mimea pamoja na viumbe vilivyoko ndiyo roho za watu na ni jukumu la kila mmoja kuyalinda na kuyaendeleza.

Kwa kauli yake jamii inapaswa kuelewa na kuzingatia utekelezaji wa sheria za mazingira zilizoko kwa sababu licha ya kuwa na sheria bora lakini utekelezaji na usimamizi wake umekuwa tatizo na hauonekani.

Kwa mfano Sheria za Mazingira za Tanzania na nyingine ndogo za halmashauri ziendelee kusimamiwa kwa kupiga faini wanaoharibu misitu, vyanzo vya maji, kulisha mifugo barabarani na kuchoma mashamba na mapori.

Siku ya Mazingira Duniani iliyofanyika jijini Dodoma ilikuwa na kauli mbiu "Tanzania ni moja tu, tunza mazingira".

## Marekani kusaidia maeneo matano ajira wanaohitimu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI ya Marekani imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania katika maeneo matano yatakayosaidia vijana kujiajiri wanapohitimu masomo.

Maeneo hayo ni elimu, afya, biashara na uwekezaji, usalama na utawala bora.

Pia, imeipongeza serikali ya awamu ya sita kutokana na kufanya maridhiano na vyama vya siasa na kutominya uhuru wa vyombo vya habari.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright, alisema hayo alipokuwa akizungumza kwenye mdahalo wa maadhimisho ya miaka 60 ya ushirikiano baina ya Marekani na Tanzania yaliyofanyika, jijini Dodoma.

Balozi Wright alisema nguzo kuu zinazodumisha uhusiano huo ni pamoja na kuwawezesha vijana kutumia na kunufaika na fursa zitakazojitokeza siku zijazo, kuongeza biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo, kuimarisha amani na usalama katika kanda na taasisi za kidemokrasia ili wananchi wote waweze kushiriki kikamilifu katika mchakato wa utawala.

Alisema Serikali ya Marekani imedhamiria kuhakikisha vijana wa Tanzania wana afya, elimu nzuri pamoja na ujuzi utakaowawezesha kuzitumia fursa vizuri za kiuchumi zitakazojitokeza.

Alisema sehemu kubwa ya msaada wa maendeleo wa Marekani kwa Tanzania umeelekezwa katika programu za kusaidia afya na elimu kwa vijana.

Alisema wanafanya hivyo kwa sababu wanaamini mafanikio huanza katika umri mdogo.

"Hivi karibuni tulitangaza kuzinduliwa kwa mradi wa Afya Yangu wenye thamani ya Dola za Marekani Sh. milioni 250, utakaotekelezwa kupitia USAID kwa kuboresha afya ya mama na mtoto," alisema Balozi Wright.

Alisema katika sekta ya elimu Marekani inafanya uwekezaji mkubwa ili vijana wa Tanzania wapate msingi wa elimu bora toka wakiwa wadogo, katika miaka mitano iliyopita wamechangia zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 65 ili kusaidia mfumo wa elimu ya kitanzania hususani kwenye programu ya kusoma, kuandika na kuhesabu kwa madarasa.

Alisema Tanzania ina fursa nyingi na uwekezaji ukifanyika, vijana wanaochipukia wataajiriwa pamoja na kujiajiri wenyewe kupitia fursa zilizopo ndani ya Tanzania.

Kwa upande wake, mgeni rasmi Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema serikali itaendelea kusisitiza suala la utafiti kwa vyuo vikuu ili kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.

Aliishukuru Serikali ya Marekani kutokana na ushirikiano wanaotoa katika masuala mbalimbali, hususani ya elimu, afya na uwekezaji ambao utazidi kusaidia vijana na taifa kujiinua kiuchumi.

## Atoroka nyumbani kisa kufeli masomo

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu Shule ya Sekondari Migombani, Dorice Venance (16), anadaiwa kutoroka nyumbani kwao Tabata Segerea tangu Juni 4, mwaka huu kwa madai ya kufanya vibaya kwenye masomo yake.


Baba mkubwa wa mwanafunzi huyo, Charles Kenyela, aliyefika katika ofisi za Nipashe, zilizopo Mikocheni, jijini Dar es Salaam, alisema Dorice aliondoka nyumbani siku hiyo saa tano usiku, akiwa amevaa shati la rangi ya kahawia na suruali ya kulalia ya bluu.

Alisema alimtoa nyumbani kwao Mwanza baada ya kumaliza elimu ya msingi na kumhamishia Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea na masomo ya sekondari ili kumpa msaada wa kielimu.

"Hivi karibuni alishawahi kuniambia kuwa anaomba nimrudishe nyumbani kwao Mwanza kwa sababu anahisi kuwa anapoteza muda kutokana na kufeli mitihani yake kadiri siku zinavyokwenda," alisema.

Hata hivyo, alisema alimtia moyo na kumshauri aongeze bidii kwa sababu elimu ya kijijini aliposoma msingi ni tofauti na mjini, lakini Jumatano ya wiki iliyopita mtoto huyo alitoroka usiku.

"Tuligundua kuwa ametoroka baada ya kukuta funguo zikining'inia mlangoni na tulipotazama kwenye kamera za CCTV tukamuona alivyokuwa anatoka. Mpaka sasa inakaribia wiki nyumbani kwao Mwanza hajafika na wala hapa nyumbani hayupo," alisema.



Alisema ameshatoa taarifa Kituo cha Polisi cha Tabata na kupewa RB Na. TBT/RB/2635/2022 kwa yeyote atakayemuona atoe taarifa kwenye kituo hicho au kupiga simu namba **0754485911** au **0743608494.**

# Wadau wapewa jukumu la usalama wa chakula

**Na Jenifer Gilla**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Johanes Maganga, amesema wadau wa chakula nchini ikiwamo wazalishaji, wasindikaji, wasafirishaji, wasambazaji, wauzaji na waandaaji wana jukumu la kuhakikisha kuna usalama wa chakula ili kulinda afya ya mlaji.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam kwenye maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, inayofanyika Juni 7, kila mwaka ikiambatana na kaulimbiu 'Chakula salama, afya bora'.

Alisema vihatarishi vipo katika kila hatua ya mnyororo wa chakula na kuwapo kwa uwezekano wa uchafuzi na kwamba ni jukumu la kila mdau kuhakikisha chakula kinakuwa salama.

"Tabia za jamii katika uzalishaji, usafirishaji, uuzaji, uandaaji na ulaji wa chakula, miundombinu na mifumo ya uzalishaji na usambazaji wa chakula vinaweza kuepusha au kusababisha uchafuzi wa chakula dhidi ya vihatarishi, ikiwamo kemikali za sumu, vimelea vya magonjwa na taka vinavyoweza kudhuru afya ya mlaji.

"Chakula salama huokoa maisha, sio tu sehemu muhimu ya uhakika wa chakula, bali ina mchango muhimu katika kupunguza magonjwa yatokanayo na chakula kisicho salama," alisema.

Alirejea makadirio yaliyofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2015 yanayoonesha kuwa kila mwaka, zaidi ya watu milioni 600 duniani huugua na 420,000 kati yao hufa kutokana na kula chakula kisicho salama na hutokea zaidi kwa watu wenye kipato cha chini na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Alisema TBS imeweka mifumo ya kudhibiti kuhakikisha chakula kilichopo katika soko la nchini ni salama ili kuilinda jamii dhidi ya madhara yatokanayo na kula chakula kisicho salama ikiwamo kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Naye Mwakilishi kutoka Shirika la Afya Duniani, Rose Shija, alisema magonjwa yatokayo na chakula kisicho salama bado ni changamoto katika nchi nyingi ikiwamo Tanzania akirejelea watu 81 waliugua huku wanne walifariki kutokana na ugonjwa wa kimeta, Momba, mkoani Songwe kati ya Desemba 2018 na Januari 2019.

Alisema ugonjwa mwingine unaotokana na kula chakula kisicho salama ni kipindupindu na hivi karibuni uliripuka mkoani Kigoma na Katavi na jumla ya wagonjwa 226 waliripotiwa.

Alisema chakula salama ni muhimu katika kupunguza umaskini, kukuza afya bora na ustawi, na kumaliza njaa ambayo ni malengo namba moja, mbili na tatu kati ya 17 ya Ajenda ya mwaka 2030 ya Maendeleo Endelevu.

Naye Ofisa Mazingira Mwandamizi kutoka Wizara ya Afya, Josephine Kapinga, alisema wizara inayo jukumu la kuhakikisha wananchi hawapati madhara yatokanayo na kula vyakula visivyo salama.

Alisema katika kulitekeleza hilo wanashirikiana na wadau wa vyakula na wataalam wao kutoka ngazi mbalimbali za afya na mazingira kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi juu ya usalama wa chakula.

Ofisa Biashara wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Denis Mzamilu, alisema wizara inatambua mchango wa TBS katika uzimamizi wa ubora wa chakula kwa wadau wengine wa vyakula nchini.

Alisema usimamiaji wa ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini utasaidia kuyafikia masoko ya kikanda na kimataifa hivyo kukuza uchumi wa nchi hivyo ni wizara itashirikiana TBS na wadau wengine wa chakula kuhakikisha kuwa bidhaa hiyo inazalishwa kwa kiwango cha kufikia masoko hayo.

Maadhimisho ya Siku ya Chakula Salama Duniani yaliridhiwa na Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, uliofanyika Desemba 20, 2018.


**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**

**TEMEKE SUB-REGISTRY**

**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**

**AT TEMEKE**

ONE STOP JUDICIAL CENTRE PROBATE AND MATRIMONIAL CAUSES RECEIVED SIGN: NAME: DATE: 7/6/22

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 35 OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ELIALILIA ELLIE TERRY otherwise ELIALILIA TERRY, ELIALILIA ZAKAYO TERRY**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A GRANT FOR RESEALING OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY**

**ELDA ZAKAYO KAAYA, THE PETITIONER**

**GENERAL CITATION**

***Rule 75 of Probate and Administration of Estate Rules G.N No 10 of 1963)***

All persons claiming to have any interest in the estate of Elialilia Ellie Terry deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of resealing letters of administration to Elda Zakayo Kaaya.

Objections to the grant should be filed on or before the **13th day of June 2022.**

The Will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court.

**Dated at Dar es Salaam this**......06.........**day of**.....June............... **2022**

..........................................

**PETITIONER**

**Presented for filing this**..........7th..........**day of**.......June..............**2022.**

..........................................

**REGISTRY OFFICER**

216891502

# Wanafunzi wajichora tattoo kwa chelewa

Na Waandishi Wetu

KATIKA hali isiyo ya kawaida, wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtongani, Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wamekutwa wakiwa wamejichora 'tattoo' maeneo mbalimbali mwilini zenye alama za herufi za mwanzo za majina yao.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Khamis Kingai, aliiambia Nipashe jana kuwa walipata taarifa za tukio hilo na kuamua kulifuatilia japo wao wanapeleleza makosa ya kijinai.

"Hapo hakuna kosa lolote la kijinai, tulilolibaini kwa sababu kama mtu anajichora mwenyewe tattoo, hapo kuna jinai gani? Sisi tunayafanyia kazi makosa ya kijinai, tumebaini hakuna kosa lolote la kijinai ambalo tunaweza kulipeleleza au kulichukulia hatua yoyote," alisema.

Kamanda Kingai alisema hawana chochote cha kuchunguza zaidi ya kushauri suala la nidhamu shuleni.

"Kama alivyofanya Mwalimu Mkuu wa Shule hii amewaita wazazi na kuwaelekeza kwamba kitu kilichofanyika hakiko sawasawa hizo ni hatua za huko, kijinai hatuoni kama kuna kosa la mtu kujichora tattoo kwenye mwili wake.

"Amejichora mwenyewe halafu siyo kwamba ni mtu amelazimishwa, siyo kwamba amejeruhiwa kwa kuchomwa moto, ametaka mwenyewe amejichora alama hatujaona kama kuna kosa lolote la kijinai hapo."

Ofisa Elimu Msingi Manispaa ya Kinondoni, Theresia Kyaria, akizungumza juzi na chombo kimoja cha habari (siyo Nipashe), alisema ni wanafunzi wachache kati ya 1,950 waliopo shuleni hapo, hawazidi 25 ambao wamejichora wenyewe tattoo kwa kutumia chelewa.

Alisema taarifa walizipata siku ya tukio wakati walimu wakifanya ukaguzi wa kawaida kwa wanafunzi na wakabaini baadhi yao wamechora kwenye mikono na siyo wote walichora herufi za kufanana.

"Kila mtoto alikuwa anaandika herufi ya jina lake la kwanza na la mzazi wake la kwanza, herufi zinatofautiana na wengine wamechora kwenye mikono na baadhi kwenye mapaja.

"Tumechukua hatua nyingi kupitia polisi kata dawati la jinsia, elimu msingi tumefanya uchunguzi kujua, vyombo ambavyo ni polisi ni kwa nini na tukio limeanzaje, wakabaini kuna mtoto mmoja msichana wa kazi wa nyumbani kwao wamejichora tattoo, mtoto alipomwona aliona inapendeza akaenda shuleni akachora," alisimulia. Alisema mtoto huyo alipofika shule aliwaambia wenzake kwamba dada yake amejichora ndipo naye akajichora na kwa sababu ana rangi nyeupe, wenzake waliona amependeza ndipo walipoingia kwenye mkumbo.

"Tulibaini baadhi wana vidonda ndipo wakapelekwa kituo cha afya kwa matibabu kwanza ili vidonda vipone na pili kuangalia kama kuna athari zozote za kiafya wamepata. Tumebaini hakuna athari zozote za kiafya, wachache ambao walikuwa na vidonda vilitibiwa na wameshapona," alisema.

Kiongozi huyo alisema Juni 4, mwaka huu, walikuwa na kikao kati yao na wazazi takribani 600 na wamekubaliana mambo mbalimbali likiwamo hilo la namna ya kuwasaidia watoto waondokane na matendo ambayo hayafai na yasiyo na tija katika jamii.

Pia alisema polisi inaendelea na taratibu zao za uchunguzi wa kujiridhisha kuhusiana na tukio hilo.

"Ustawi wa jamii wanaendelea kutoa elimu, idara ya elimu kupitia kitengo cha elimu ya watu wazima wapo kule wakiendelea kuelimisha watoto siyo shule ile tu na nyingine za Manispaa," alisema.

Alisema tukio hilo halina uhusiano wowote na imani za kishirikiana, akisema: "Tumekwenda hadi nyumbani kwa watoto, baadhi tumeona ni kundi tu yaani mtoto anaiga."



Mkurugenzi wa kitengo cha dijitali na huduma za ziada Vodacom Tanzania Plc, Nguvu Kamando (katikati), akipokea tuzo ya kampuni ya mawasiliano ya simu yenye ubunifu kwa 2021 kutoka kwa Ofisa Uendeshaji wa Serengeti Bytes, Michael Mallya, jijini Dar es Salaam jana, ambapo Vodacom walishinda tuzo hiyo kutokana na uwekezaji wake na uboreshaji wa mtandao na huduma bora kuzidi makampuni mengine ya mawasiliano kwenye tuzo za Tanzania Digital Awards zilizoandaliwa na Serengeti Bytes. Kulia ni Mkurugenzi wa huduma kwa wateja Vodacom, Harriet Lwakatare. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machifu waagizwa kutoa elimu sensa

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, amewaomba machifu wa kabila la Kisukuma mkoani hapo, kutoa elimu kwa jamii ili kuondoa imani potofu kuhusu sensa ya watu na makazi.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa na imani potofu ya kuhesabiwa kwa madai kuwa watoto wao wakihesabiwa ni mkosi ndani ya familia. Alibainisha hayo juzi wakati alipowasili kuzindua tamasha la utamaduni akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema malengo ya serikali kwenye sensa ni kutaka kujua idadi ya watu wake kamili kwa kila eneo ili kurahisisha mipango yake ya maendeleo kwa kupeleka mahitaji sahihi ya wananchi katika eneo husika kulingana na idadi yao.

"Machifu tunawaomba mtusaidie kuelimisha jamii juu ya zoezi hili la kuhesabiwa sensa ya watu na makazi, msaidieni mkuu wenu Chifu Hangaya kuondoa imani hizi potofu kuwa wakihesabiwa watoto ni mkosi ndani ya familia, hakuna ukweli wowote juu ya imani hii," alisema Dk. Chana.Katika hatua nyingine, aliwasihi machifu kupitia tamasha hilo la utamaduni watoe elimu kwa vijana ili waishi kwa kuenzi mababu zao kwa kudumisha amani na kuishi katika misingi mizuri hatua ambayo itasaidia kupunguza mmomonyoka wa maadili kwa vijana hususani kizazi kipya. Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa umoja wa machifu nchini, Nyamilonda Mikomangwa, aliahidi kumuunga mkono Chifu Hangaya (Rais Samia) kwa kuelimisha jamii katika himaya zao za kimila na wananchi wote ili washiriki sensa.

Alisema machifu wanampongeza Rais Samia kwa kutengeneza filamu ya Royal Tour ambayo imetangaza mambo ya utalii na utamaduni nchini na kutoa fursa mbalimbali za kiuchumi.

Naye Mwenyekiti wa machifu mkoani Shinyanga, Charles Njange, aliiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara kwenye maeneo ya vivutio ili yafikike kwa urahisi.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema wameandaa tamasha hilo la utamaduni ili kutekeleza agizo la Rais Samia kuendeleza utamaduni wa Mtanzania na kutangaza utalii wa ndani kupitia vivutio vya kitamaduni vilivyoko mkoani humo.

Alisema tamasha hilo litakuwa endelevu na wananchi wa mkoani humo watakuwa wakifika kwenye kijiji hicho ambacho kimetengenezwa katika eneo la Butulwa Oldshinyanga, kujifunza mambo mbalimbali ya mila na desturi za kabila lao.

Kaulimbiu ya tamasha hilo inasema "Utamaduni wetu, urithi wetu, jiandae kuhesabiwa."

## Taasisi 12 kufungua huduma pamoja

Na Idda Mushi, MOROGORO

TAASISI 12 zimeungana kufungua dirisha la pamoja litakalowezesha wawekezaji kupata huduma zote sehemu moja kwa majaribio litafunguliwa rasmi Juni 15, mwaka huu.

Muunganiko wa taasisi hizo umekuja baada ya kubainika changamoto kubwa kwa wawekezaji kutumia muda mrefu na kuzungukia taasisi zaidi ya moja ili kupata huduma jambo linalochelewesha shughuli za uwekezaji.

Mkurugenzi wa Utafiti, Mipango na Mifumo ya Taarifa kutoka kituo cha Taifa cha Uwekezaji, Maftaa Bunini, alisema serikali imeamua kufanya hivyo ili kuboresha huduma ya uwekezaji hasa kwa kutumia Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kuandaa mfumo huo wa pamoja.

Alisema hayo baada ya wakuu wa taasisi 12 zinazohusika na utoaji wa vibali kwa wawekezaji kukutana mjini hapa na kwamba mfumo huo wa Tanzania Electronic Investment Window (Single Window), utawawezesha wawekezaji kupata huduma mbalimbali katika eneo moja ikiwamo cheti cha vivutio vya uwekezaji, usajili wa kampuni, namba ya mlipa kodi, vibali vya kuishi na kuwekeza nchini na huduma zingine.

"Kwa sasa wataalamu wanaukamilisha mpango huu na matarajio ni kuanza Juni 15, 2022 kwa majaribio na kwa matumizi ya ndani utakuwa umekamilika na serikali itaweza kuuzindua rasmi wakati wowote," alisema Bunini.

Kwa upande wake, Meneja mradi wa Mfumo wa Single Window, Robert Mtendamema, alisema taasisi hizo zinatengeneza dirisha moja ambalo litamwezesha mwekezaji akiingia kwenye mfumo aweze kupata vibali mbalimbali vya uwekezaji kwa haraka na utawasaidia kupata vyote kwa pamoja na kuacha kufuata kila kimoja kwenye taasisi yake.

"Manufaa yake ni makubwa kwa mwekezaji kwani hakutakuwa na urasimu wa kwenda kuzungukia kila taasisi kwa siku tatu hadi tano au zaidi na kuchukua muda mrefu kupata huduma, badala yake huduma zimerahisishwa," alisema.

Kamishna wa Uhamiaji nchini, Dk. Anna Makakala, alisema mfumo huo utasaidia na kuwapa fursa wageni, watalii na wawekezaji popote walipo kuingia kwenye dirisha moja kupata huduma za taasisi zote ambazo anatakiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango nchini (TBS), Dk. Yusuph Ngenya, alisema ndani ya mfumo huo wataingia katika hatua ya pili baada ya mwekezaji kuwekeza.

"Kama mwekezaji atakuwa anatengeneza bidhaa, hapo sasa tutaingia kuhakikisha bidhaa yake ni safi na salama, ambapo sisi tutaingia sasa kwenye awamu ya pili, tunaweza kumwambia alete bidhaa kuipima au tukamfuata, kwa sasa tuna mfumo wetu ambao kero zimeondoka," alisema Dk. Ngenya.

# DART, TanTrade kupeleka mwendokasi Sabasaba

Na Joseph Mwendapole

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umetiliana saini makubaliano ya ushirikiano na Mamlaka ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa ajili ya kupeleka usafiri wa mabasi yaendayo haraka katika maonyesho ya kimataifa ya biashara, maarufu Sabasaba, ili kuwarahisishia wananchi usafiri katika msimu wa maonyesho.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, alibainisha hayo jana alipozungumza katika hafla ya kutiliana saini makubaliano hayo iliyofanyika katika ofisi za TanTrade Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam.

Alisema uamuzi wa kupeleka mabasi katika viwanja vya Sabasaba ni mwendelezo wa mkakati wa kutatua kero ya usafiri wa umma katika Mkoa wa Dar es Salaam hasa katika eneo la Mbagala na maeneo ya jirani.

Dk. Mhede alisema kupeleka mabasi katika viwanja vya Sabasaba pia ni kutekeleza maagizo ya Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ambayo ilifanya ziara hivi karibuni katika wakala kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na kutoa agizo hilo.

"Uamuzi wa kuleta mabasi huku Sabasaba ni wa kimkakati kabisa na ni mwanzo wa kuelekea kuleta huduma kamili ya mabasi katika Barabara ya Kilwa itakapokamilika mwezi Machi mwakani na niwahahakikishie wakazi wa Mbagala na maeneo ya jirani kuwa usafiri unaanza kuja wakati wa Sabasaba na muda si mrefu mkandarasi akikamilisha barabara tutaanza huduma rasmi na kwa viwango vya kimataifa kuliko ilivyokuwa katika awamu ya kwanza," alisema.

Alisema maonyesho ya Sabasaba ni sehemu ambayo inakutanisha watu wengi kutoka sehemu mbalimbali za jiji, hivyo wakala umeona ni vyema kutumia fursa hiyo kuwarahisishia usafiri lakini pia kutangaza huduma. Katika siku za usoni taasisi hizo pia zimekubaliana kuendeleza ushirikiano ikizingatiwa maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka yanakwenda sanjari na kuboresha miundombinu na makazi yanayaopakana nayo kwa ajili ya kutumia fursa zitokanazo na miundombinu hiyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Mohamed Hamis, alisema makubaliano baina yake na DART ni mwanzo wa kuendeleza kutangaza shughuli za biashara katika viwanja vya Sabasaba lakini pia ni mwanzo wa kupanua wigo wa shughuli za uchumi katika maeneo yanayozunguka viwanja hivyo.

"Kuendelea kupanuka kwa maendeleo katika eneo hili ni dhahiri kuwa hata shughuli za kiuchumi hususan biashara zitaongezeka hivyo wenzetu wakileta mabasi huku kwetu wataongeza thamani katika ustawi wa jamii inayotuzunguka kwani usafiri katika eneo hili ni changamoto kubwa," alisema.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha maonyesho ya mwaka huu, DART itapeleka mabasi zaidi ya 10 ambayo yatatoa huduma kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa mbili usiku.

Alisema wananchi watanunua tiketi za kuingia kwenye maonyesho ya Sabasaba wakiwa katika vituo vya mwendokasi vya Kimara, Kivukoni, Morocco, Gerezani na hata Kibaha, Mloganzila na Mbezi kama kutakuwa na uhitaji huo. Alisema watumiaji wa Mabasi Yaendayo Haraka kutoka maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam wamerahisishiwa pia namna ya kuingia katika viwanja vya Sabasaba ambapo kimeandaliwa kituo maalum ambacho kiko nje ya viwanja hivyo na wananchi watakaposhuka tu hawatalazimika kukata tiketi watatumia tiketi walizokatia katika vituo mbalimbali vya DART.

Alisema sanjari na wananchi kurahisishiwa ukataji tiketi za kuingia sabasaba pamoja na kuwepo na huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka wametengenezewa pia mlango wao maalum ambapo wakishuka tu kwenye mabasi wanaingia uwanjani moja kwa moja bila usumbufu.

Kadhalika, alisema kutakuwa na huduma ya bure ya mtandao wa WiFi katika mabasi na katika maeneo yote ya viwanja vya Sabasaba.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Afroil, Lufti Binkleb (wapili kushoto) na Meneja mtaalamu wa vilaishi wa Kampuni ya Toyota Tanzania, Anam Mwemutsi, wakibadilishana mikataba, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano ya kuuza vilainishi vya Toyota Genuine Motor Oil, katika vituo vya mafuta vya Afroil. Kushoto ni Meneja Masoko wa Toyota Tanzania, Nadah Dhijebi na Meneja Mauzo na Masoko wa kampuni ya Afroil, Erasmo Nyoni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Watoto miguu vifundo wanatibika wapelekwe hospitali

Na Yasmine Protace

WATOTO 300,000 katika vizazi hai huzaliwa na miguu vifundo kila mwaka nchini Tanzania.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu Hospitali ya CCBRT, Cyprian Nyomoka, jijini Dar es Salaam, wakati akitoa taarifa katika maadhimidho ya Siku ya Miguu Kifundo, ambayo kila mwaka hufanyika Juni 3.

"Watoto laki nane katika vizazi hai, huzaliwa kila mwaka duniani wakiwa na miguu vifundo, huku Tanzania watoto laki tatu kwa mwaka huzaliwa wakiwa na miguu vifundo," alisema.

Alisema changamoto ni baadhi ya wazazi kutofika kwa wakati hospitalini CCBRT kuwapeleka watoto kupatiwa matibabu.

Alisema matibabu yanachukua miaka mpaka mitano, mtoto kurudi miguu katika hali yake ya kawaida, lakini inatakiwa mzazi afike kliniki kila anapopangiwa, kama asipohudhuria vizuri hawezi kupona.

"Mtoto aletwe mapema CCBRT ili aweze kufanyiwa matibabu na kupona kama anachelewesshwa kupatiwa matibabu uponaji wake unakuwa mgumu," alisisitiza.

Vilevile, alisema wanawashukuru Miracoseet, kwa kuwafadhili fedha ili waweze kutoa huduma bure kwa watoto ambao wanafika kupata matibabu ya miguu kifundo.

Alisema hali ya uchumi kwa baadhi ya wazazi ni tatizo linalosababisha wazazi kushindwa kupata nauli za kutoka maeneo waliopo kufika hospitali kwa matibabu.

Kwa mujibu wa Nyomoka, CCBRT ilianza kutoa matibabu ya miguu kifundo tangu mwaka 2001.

# OreCorp yaahidi kutunza mazingira

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya OreCorp imesema itaendelea kujizatiti katika kuhakikisha inatekeleza shughuli zake kwa kufuata kanuni zinazokubalika duniani katika utunzaji wa mazingira kwa kupunguza athari za kimazingira.

Taarifa iliyotolewa juzi na Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Damien Valente, ilibainisha kuwa kampuni hiyo inajivunia ushiriki wake katika Siku ya Mazingira Duniani na kwa maendeleo ya Wilaya ya Sengerema.

"Ninafuraha sana juu ya mpango huu unaotekelezwa na Meneja Mazingira wa Mradi wa Dhahabu wa Nyanzaga, Delphinus Kaballega, ambao unatukumbusha kuwa tunahitaji kubadilisha mitindo yetu ya maisha kwa manufaa ya sayari yetu na kwa ajili ya kila mmoja," alisema Valente.

Alisema kama sehemu ya kujituma kwao kwenye ajenda ya Taifa na kwa wakazi wa Kijiji cha Ngoma, kampuni ya OreCorp imekuwa ikishiriki kufanya usafi wa mazingira kwa kushirikiana na jamii inayoishi karibu na eneo la Mradi wa Nyanzaga.

"OreCorp inaendelea kujizatiti katika kuhakikisha inatekeleza shughuli zake kwa kufuata kanuni zinazokubalika duniani kote katika utunzaji wa mazingira kwa kupunguza athari za kimazingira zinazoweza kutokea kutokana na shughuli za kampuni.

"Kama sehemu ya kujituma, OreCorp inatarajia kuwa na ufanisi zaidi kimazingira wakati wa utekelezaji wa shughuli zake ili kuhakikisha mazingira yanakuwa salama kwa jamii inayozunguka eneo la mradi," alisema.

Aliongeza kuwa mpango huu unakuja katika kipindi muhimu kwa kampuni kufuatia kutolewa kwa leseni maalum ya uchimbaji madini Desemba 13, mwaka jana, kwa kampuni ya uchimbaji madini ya Sotta (SMCL), inayotokana na ushirikiano baina ya serikali asilimia 16 na OreCorp asilimia 84, kujenga mradi wa Mgodi wa Dhahabu wa Nyanzaga wenye thamani ya Sh. bilioni 670, kusini mwa Kijiji cha Ngoma wilayani Sengerema.

Alisema mradi huo uko mbioni kuwa mgodi mkubwa zaidi wa kwanza wa dhahabu kuwahi kujengwa Tanzania kwa zaidi ya muongo mmoja na wa kwanza kuwahi kujengwa wilayani Sengerema.

Valente alisema Mradi wa Dhahabu wa Nyanzaga upo Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza kwenye ukanda wa dhahabu wa Ziwa Victoria, unakadiriwa kuwa na wakia milioni tatu za dhahabu na utazalisha kiasi cha wakia tani sita za dhahabu kwa mwaka na ujenzi wake utagharimu Sh. bilioni 670.

Alisema mradi huo pia utazalisha ajira muhimu na kuchangia uchumi kupitia ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, mirabaha na kodi, kwamba utaleta faida za ziada kwa mkoa kama vile elimu, vituo vya afya na miundombinu kupitia miradi wezeshi inayofanywa na kampuni hiyo kwa lengo la kuinufaisha jamii.

# Serikali mbioni kulipa fidia waliopisha upanuzi JNIA

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa iko katika hatua za mwisho za kufanya uthamini mpya kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wote wa Kipunguni waliopisha upanuzi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Segerea (CCM), Bonna Kamoli.

Mbunge huyo alihoji kauli ya Serikali kuhusu wananchi wa Kipunguni ambao wamezuiwa kuendeleza maeneo yao tangu mwaka 1997 kwa lengo la kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege huo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mwakibete, alisema Serikali ipo katika hatua za mwisho za kufanya uthamini mpya na zoezi hilo linatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2022.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alihoji ni lini wananchi hao watapata barua ya kujulishwa kwamba wanafanyiwa tathmini upya.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema tayari Serikali imeshaandika barua kwenda Jiji la Dar es Salaam tangu mwezi Aprili mwaka huu ambao wana wajibu wa kuwajulisha wananchi kwamba zoezi hilo linaanza rasmi.

"Zoezi lenyewe litaanza mwezi Julai na litakamilika Septemba mwaka huu 2022," alisema.

Katika swali lingine la nyongeza, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi (CCM), Bakar Hamad Bakar, alihoji fedha zilizotengwa kwenye Uwanja wa Ndege Pemba zimejumuisha fedha za fidia za wananchi watakaopisha maeneo yao.

Naibu waziri huyo, akijibu swali hilo, alisema katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2022/23, serikali imetenga fedha kwa ajili ya upanuzi wa uwanja huo na kulipa fidia kwenye eneo litakalochukuliwa kwa ajili ya ujenzi.

Katika swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Jesca Kishoa, alihoji sababu za kuchelewa kuanza uboreshaji wa Uwanja wa Ndege Singida ambao kwa muda mrefu wananchi wa Singida wamepisha maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wake.

Mwakibete, akijibu swali hilo, alisema kwa mwaka wa fedha ujao, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya tathmini ya uwanja huo.



Mbunge wa Bukene, Selemani Zedi, akiuliza swali kuhusu lini zahanati ya kijiji cha Sojo, itapandishwa hadhi kuwa kituo cha afya, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge wakunwa miradi maji miji 28

WABUNGE wameipongeza Serikali kwa kutafuta fedha za kutekeleza miradi ya maji katika miji 28 nchini.

Pongezi hizo zilitolewa jana kwa nyakati tofauti na wabunge mbalimbali walipokuwa wakiuliza maswali ya masuala ya maji kwenye maeneo yao.

Miongoni mwa wabunge hao, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alipongeza Serikali kwa kusaini mkataba wa utekelezaji wa miradi hiyo ikiwamo wa Makonde mkataba ulitiwa saini juzi.

"Ninapenda kushukuru kuna mradi mkubwa wa utoaji maji Mto Ruvuma kutoka Kijiji cha Maembe chini kupeleka Manispaa ya Mtwara, mradi ambao utanufaisha Jimbo la Nanyamba, Mtwara Vijijini na Manispaa ya Mtwara. Je, mradi unatekelezwa lini?" alihoji.

Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alitaka kujua kauli ya Serikali kuhusu Tarime kama ipo miongoni mwa miji hiyo 28.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alisema kuwa juzi Rais Samia Suluhu Hassan alifanya jambo zito la kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa mradi wa Mto Ruvuma, ni mkakati wa wizara na itahakikisha maji ya mto huo yatakwenda kutatua kero iliyopo kwenye maeneo yatakayopitiwa na utekelezaji wake utafanyika mara baada ya Serikali kupata fedha.

Kuhusu Tarime, Naibu Waziri huyo alisema Rorya-Tarime ipo miongoni mwa miji hiyo huku Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akikazia na kuwatoa wasiwasi wabunge kuwa Tarime ipo kwenye miji hiyo.

Awali, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bupe Mwakang'ata, alihoji lini mradi wa maji wa Ikozi uliopo Sumbawanga Vijijini utakamilika.

Akijibu swali hilo, Mahundi alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Ikozi utakaohudumia vijiji vya Ikozi, Kazwila, Chituo na Tentula vya Kata ya Ikozi, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini.

Alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa bwawa, ulazaji wa bomba kuu umbali wa Kilometa 1.2, nyumba ya mtambo, ununuzi na ufungaji wa pampu za kusukuma maji na ujenzi wa mfumo wa kusafisha na kutibu maji.

Naibu waziri huyo alisema utekelezaji wa mradi utakamilika katika mwaka wa fedha 2022/23.

# Yatakiwa kutoa rukuzu miche ya michikichi

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Slyvia Sigula, ameitaka serikali kutoa ruzuku ya miche ya michikichi kwenye Vyama vya Ushirika mkoani Kigoma kwa kuwa sasa mche mmoja unauzwa Sh. 5,000.

Akiulizwa swali la nyongeza bungeni jijini hapa jana, mbunge huyo alisema kutokana na uhaba wa mafuta ya kula nchini na hamasa iliyofanywa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wananchi wa Kigoma wamehamasika kuingia kwenye zao la michikichi.

"Lakini kumekuwapo na uhaba wa upatikanaji miche ya michikichi imefikia hatua mche mmoja unauzwa kwa Sh. 5,000. Je, serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa vyama vya ushirika?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema maelekezo ya Waziri Mkuu ni kwamba wizara hiyo itoe miche bora ya michikichi kwa wakulima wa Kigoma na kwamba wanaendelea kwa sasa kutoa miche hiyo katika Kambi ya JKT Bulombora na Gereza la Kitwanga.

Alisema miche iliyozalishwa hadi sasa ni milioni tisa na tayari miche iliyogawiwa kwa wananchi ni 970,000 na kwamba miche hiyo inatolewa bure kwa wakulima kwa sharti la kwamba wawe kwenye mashamba makubwa ili kurahisisha ufuatiliaji.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji lini Vyama vya Maendeleo ya Ushirika vya zao la mchikichi vitaanza kufanya kazi katika Mkoa wa Kigoma.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema Mkoa wa Kigoma una Vyama vya Msingi vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) 14 vya zao la michikichi.

"Katika Halmashauri za Wilaya za Kigoma (9), Kigoma Manispaa (2), Uvinza (2) na Buhingwe (1) ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuendeleza zao la michikichi,"alisema.

Aidha, alisema vyama hivyo vimeshaanza kufanya kazi na kwa sasa vipo katika hatua ya kupata mkopo wa Sh. bilioni 2.9 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) utakaowezesha kuboresha mashamba ya wakulima, miundombinu ya uhifadhi mikungu ya michikichi, mashine za uchakataji na ukamuaji wa mafuta ya mawese.




Habari zote na Augusta Njoji

MEMBE: SIBANDUKI TENA CCM HADI NIFE
Ukurasa 14





Ukurasa 13

**UCHAGUZI WA KENYA**
**Tume yapuliza kipenga**

siasa
JUMATANO JUNI 8, 2022
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

SAFARI YA MAPINDUZI KISIASA...

# Maridhiano yanapoibua pongezi za Lissu, Mbowe kuteta na Rais Samia

- Historia ya yanayofanyika yatibu majeraha
- Simulizi za Unguja, Kenya kipekee marejeo

**Na Peter Orwa**

KIMSINGI, suala la maridhiano katika mustakabali wa kisiasa si jambo geni kwenye ulingo wa kisiasa na ndio imetawala katika sura nyingi ndani ya mataifa mengi, yakiwamo ya Afrika Mashariki.

Ikirejewa tafsiri ya kamusi ya Kiswahili nchini, mzizi wake unaanzia katika neno 'ridhia' ambayo kamusi hiyo inaorodhesha matendo kama; kutoa ruhusa kitu kifanyike, kubali, hiari na kuidhinisha.

Pia, ni tafsiri inayoenda mbali penye msamiati 'maridhio' unaobeba ufafanuzi:"Mambo ambayo mtu amekubaliana nayo." Kwa hilo, ndani ya siasa za nchi hasa awamu iliyopo ya uongozi wa kitaifa, ni jambo linaloendelea kuchukua sura pana katika mamlaka ya uongozi wa nchi, kukishuhudiwa hatua zake kwa yaliyo rasmi na yasiyo rasmi kufanyika.

Inaporejewa kwa kina kamusi ya kimataifa iitwayo Collins inayobeba tafsiri ya neno maridhiano kwamba ni: "Hali ambayo (watu) wanakubaliana na jambo ambalo liko katika mazingira halisi, au utashi wao, ili kuendana nayo sawa, au wanafikia utashi huo kutoa fursa ya kukubalika kwa utashi wa wenzake."

Nadharia za sayansi ya siasa na maandiko yake mbalimbali yanagusa dhana kwamba, ili kuwepo mafanikio na ubora wa utawala kisiasa, kuna ulazima mambo kadhaa yakajumuishwa uwepo wake yakiwamo; utawala uliopo ukubalike kwa umma, vivyo uendane na kuwapo utawala bora.



Rais Samia Suluhu Hassan, alipokutana na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, mnamo Februari 16 mwaka huu, jijini Brussels, Ubelgiji. **PICHA: MTANDAO**

Ndipo kutashuhudiwa utawala unaungwa mkono kwa kiasi kikubwa, pasipo kulazimishana. Ni mafanikio ambayo kwa kiasi kunahitaji dhana ya 'maridhiano' yanayochukua nafasi, hata kushuhudiwe umma kukubaliana.

Mara zote mtazamo na mustakabali wake, unarejea upepo wa siasa nchini kuhusu maridhiano yanayoendelea kufanyika kila kukicha. Mathalan, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Hassan Mwinyi anapoweka msimamo wake kukubaliana katika usimamizi wa kisiasa anaotumikia na kuwekwa kando kilichowafanya wavutane huko nyuma.

Itakumbukwa katika siku zake za mwanzo tu za siasa nchini, Rais Dk. Mwinyi akatamka anakosimamia kwamba "huu si wakati wa kufukua makaburi," akimaanisha kusahau misuguano iliyopita na kujikita pamoja kuijenga Zanzibar.

Hadi sasa kuna ushuhuda wa sura ya mafanikio makubwa kisiasa na nyendo za maendeleo, ikiwamo kinachojulikana sasa 'Uchumi wa Buluu' kujaza ngazi ya kinachofanyika kiuchumi katika sekta za utalii na kilimo cha karafuu visiwani na kamwe si msuguano.

**ANAKOPITA RAIS SAMIA**

Kwa Serikali ya Muungano, Rais Samia Suluhu Hassan, ametumia njia nyingi katika mantiki hiyo ya usuluhisho, akiamua mambo kadhaa ya kiutawala ngazi ya kitaifa na kukashuhudiwa mengi yakiridhiwa yenye sura ya umoja wa umma uliopo.

Msingi wake kimantiki, Rais Samia kwa kiasi kikubwa iko katika ambacho amekuwa akikitambulisha, pia matendo yake yana falsafa ya uongozi wa maneno kidogo, ila wenye maono, tafsiri na msimamo wa kina katika anachokifuatilia katika uongozi, sura ya pili nyuma ya pazia akiangalia mbali na hulka ya uzazi, katika yale anayotekeleza.

Ni katika staili hiyo ya uongozi hadi sasa kunashuhudiwa watuhumiwa wengi wa kisiasa wameachiwa huru kupitia kanuni ya kisheria ya serikali kutokuwa na haja ya kuendelea na baadhi ya kesi, ikiwamo uamuzi uliofanywa na serikali siku chache zilizopita.

Mara tu baada ya kufutiwa mashtaka mwaka huu na kutolewa rumande gerezani, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akakutana na Rais Samia na baada ya kipindi si kirefu akiwa na ujumbe wake, akakutana tena na Rais Samia, wakiambatana na wajumbe wa chama chake kujadiliana.

Ni uamuzi ulioshangaza wengi, lakini Mbowe akautetea kwamba ni fursa nyeti ambayo hakuwa tayari kuikosa, kwani ni ajenda yake ya muda mrefu, hata kabla ya kuingia jela .

Kisiasa, inaonekana kuwapo sura pana ya maridhiano kutoka chama hicho. Katika kikao chake cha uongozi kilichofanyika mjini Iringa, akaweka bayana ni nafasi aliyoitafuta sana wakati wote, kipindi ambacho CHADEMA imejiweka kando ikilalamikia mengi kisiasa.

Mbowe akakiambia kikao hicho cha wajumbe kinamaana kitaifa kwa chama chake, kwamba amefurahia kupata fursa ya kukutana na mkuu huyo wa nchi kujadili mustakabali wao, huku mwishoni mwa wiki iliyopita akifafanua sasa anaona nuru ya maridhiano kati ya chama chake na uongozi wa kiserikali.

Ni mustakabali ambao siku mbili kabla ya matamshi ya Mwenyekiti Mbowe, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, ambaye sasa anaishi nje ya nchi, Ubelgiji, naye anakiri kuna ishara ya kutendewa haki na uongozi wa serikali madarakani.

Lissu, aliyekwishakuwa mbunge na mgombea urais kwa tiketi ya

INAENDELEA UK.12

### 50/50 KATIKA UONGOZI

# Mwangaza kwa mbali unaonekana

## •Ila msururu wa vikwazo unauzuia

**Na Sabato Kasika**

LINAPOKUJA suala la usawa wa kijinsia katika uongozi na majukumu mengine, wanawake wapo mstari wa mbele kulipigania ili kuwepo na uwiano kati yao na wanaume kwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuteuliwa.

Wanapigania usawa huo, kwa kuwa uongozi hauna jinsi, awe mwanaume au mwanamke, wote wanauweza kwa vile kuongoza, si kutumia misuli na mabavu bali unategemea elimu, weledi, hekima na busara.

Katika harakati hizo za kusaka usawa wa kijinsia, watetezi wanakiri kuwa kumekuwapo na mabadiliko kwenye masuala ya uongozi na mipango madhubuti inayolenga kufikia 50/50.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anasema tangu 1997, Tanzania imeshuhudia mabadiliko kuanzia uteuzi wa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Wakili Henga anasema, kwa sasa zipo nafasi kadhaa za uongozi ambazo miaka ya nyuma hazikushikwa na wanawake, lakini leo ziko mikononi mwao.

Baadhi ya nafasi hizo ni pamoja na ya Waziri wa Ulinzi, Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu na Katibu wa Bunge na kwamba ongezeko la wanawake katika nafasi za uongozi ikiwamo baraza la mawaziri limeshuhudiwa na sasa ni 16.



Anna Henga

“Lakini pia mabalozi wanawake tisa kati ya 33, wakuu wa mikoa sita kati ya 20, wakuu wa wilaya 40 kati ya 101, wakurugenzi wa serikali za mitaa 52 kati ya 132,” anasema.

Mkurugenzi Mtendaji huyo anasema, hatua ya Tanzania kuahidi kusimamia haki za wanawake kiuchumi kwenye Baraza la Usawa wa Kijinsia Duniani, msimamo uliotolewa Juni mwaka jana ni jambo linalopokelewa kwa mikono miwili na kinamama.

“Kumekuwapo pia na mabadiliko ya sheria mbalimbali zinazolinda na kutetea haki za wanawake ikiwamo kuweka wizara mahsusi kwa masuala ya jinsia, hali inayoonyesha kuwa usawa wa kijinsia unapewa umuhimu,” anasema.

Aidha, anaongeza kuwa kumekuwapo na mipango mbalimbali yenye lengo la kumnyanyua mwanamama ikiwamo kurudisha shuleni watoto wa kike waliopata ujauzito na kuongeza shule na madarasa ili kukidhi mahitaji ya kielimu.

**VIKWAZO VILIVYOPO**

Wakili Henga anasema, pamoja na mafanikio hayo, wanawake nchini wanapitia vikwazo vingi ambavyo vimesababisha waendelee kukosa haki zao na kukwamisha juhudi za kufikia usawa wa kijinsia.

“Kwa mfano, kukithiri kwa ukatili dhidi yao, hasa ukatili wa kingono, kimwili na kiuchumi, kuendelea kuongezeka kwa mauaji ya wanawake kila kukicha ni pamoja na mambo yayochangia wengi wao kuwa hatarini,” anaonya.

Anafafanua kuwa taarifa ya haki za binadamu Tanzania ya kituo hicho ya mwaka 2020, iliripoti zaidi ya matukio 14, huku matukio 7,263 yakiwa ni ya ubakaji na mengine 26,544 ni ya ukatili dhidi ya wanawake.

“Sheria zetu bado zinamkwamisha mwanamke kama ya mirathi, ndoa na kutokuwa na sheria maalum ya ukatili wa kijinsia vimeendelea kumkandamiza mwanamke na kumnyima haki za msingi,” anasema.

Mkurugenzi huyo anaongeza kuwa utekelezaji wa sheria bado umekuwa na changamoto na kwamba hata zilizopo zingeweza kumpa ulinzi mwanamke ipasavyo na kwamba bado kuna changamoto katika utekelezaji wake.

“Ukiangalia kwenye suala la uhuru wa kiuchumi, wanawake wengi wapo kwenye wimbi la umaskini, wanashindwa kumudu kujitafutia kipato chao wenyewe suala hili linaendelea kudidimiza ustawi wa mwanamke na watoto,” anasema.

Anasema, hali hiyo inaendelea kuwaweka katika hatari za kufanyiwa ukatili, kwa kuwa hukosa maamuzi sahihi kuhusu maisha yao. Lakini pia anasema wanawake wengi hawapo katika ajira ikilinganishwa na wanaume.

“Taarifa za mwaka 2017 ya wanaume na wanawake Tanzania iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), iliripoti kuwa, katika Watanzania walioko kwenye ajira, wanawake ni asilimia 49 kulinganisha na asilimi 51 ya wanaume,” anasema.

Katika ufafanuzi wake, anasema kwa takwimu hizo, kuna kundi kubwa la wanawake ambalo bado haliko kwenye ajira, na kwamba hali hiyo inaathiriki maendeleo ya kiuchumi.

**KUKWAMA KIELIMU**

Henga anasema upatikanaji wa elimu kwa wanawake umeendelea kuwa wa kiwango kidogo ikilinganishwa na wanaume na kwamba taarifa ya NBS ya wanaume na wanawake Tanzania ya mwaka 2017, inaonyesha wanawake ambao hawajaenda shule ni asilimia 22.3 kulinganishwa na asilimia 11.3 ya wanaume.

“Hali hii inaathiri ushindani hasa katika ajira, biashara pamoja na uelewa wa masuala mbalimbali ya kijamii, ikiwamo hata masuala ya kidigitali ambayo wanawake wengi wameachwa nyuma,” anasema.

Anagusia suala la mila na desturi kandamizi kuwa baadhi ya watu wanaendelea kuzishikilia na kusababisha athari nyingi kwa wanawake kama ukeketaji, ndoa za utotoni, vipigo na kunyimwa kurithi.

“Ukiangalia ustawi wa wanawake wa vijijini wengi wanaishi huko tarkribani asilimia 77.9 ya kinamama wote Tanzania kwa mujibu wa taarifa ya NBS ya mwaka 2009 na wamekuwa wakipata athari nyingi,” anasema.

Anafafanua kuwa wanawake wanapitia changamoto nyingi na wengi wao ni wale wenye ulemavu, na wapo wanaotengwa na jamii na kukosa huduma na haki za msingi kama elimu, ajira na kushindwa kujitegemea.

“Lakini pia wanawake wenye ulemavu hubaguliwa na kufanyiwa vitendo vya ukatili vikihusishwa na imani za kishirikina, jambo ambalo watetezi wa haki za binadamu wanalipigia kelele kila wakati,” anasema.

# Maridhiano yanapoibua pongezi za Lissu, Mbowe kuteta na Rais Samia

**INATOKA UK. 11**

chama chake kwa nyakati tofauti, ameliambia gazeti hili anamshukuru Rais Samia kuagiza malipo ya mafao yake ya ubunge kati ya mwaka 2015 hadi 2019, alipotangazwa kupoteza sifa za nafasi hiyo akitumikia jimbo la Singida Mashariki.

“Nafurahi kwamba Rais Samia ameanza kurekebisha dhuluma niliyofanyiwa....,” anadokeza Lissu katika mazungumzo yake na Nipashe wikiendi iliyopita, akiendelea kufafanua:

“Ni kweli nimeshalipwa kiinua mgongo changu, bado fedha za matibabu na hizo nimeandikiwa niandike barua za kuzidai na sasa ninakusanya nyaraka zote muhimu, kwa kuwa nilitibiwa Nairobi na Ubelgiji.” Hadi sasa ameshatoa kauli inayoonyesha msimamo wa kutaka kurejea nchini karibuni.

Itakumbukwa, siku chache baada ya kupatwa mkasa wa kupigwa risasi miaka kadhaa iliyopita, akiwa nchini Kenya kwa matibabu, Mama Samia, wakati Makamu wa Rais, akiwa katika ziara ya kikazi nchini Kenya, alifika hospitalini jijini Nairobi, kumjulia hali na kwa kipindi chote amekuwa akilalamika ‘kuonewa’.

Baadaye alipohamishiwa nchini Ubelgiji kwa matibabu na akidumu kuishi huko hadi sasa, Lissu amekutana na Mama Samia akiwa ni Rais, wakazungumza mambo kadhaa, akifahamisha kupewa ushirikiano wakati huo.

**MZIZI WA MARIDHIANO**

Ni hali inayochukua sura, huku kukiwapo kumbukumbu mnamo mwanzoni mwa mwezi Aprili mwaka huu, Rais Samia amefungua Mkutano wa Kitaifa wa Haki, Amani na Maridhiano, jijini Dodoma.

Hadi sasa kuna Kikosi Kazi Maalum cha Rais, kinaendelea na kazi ya kukusanya maoni huku kukishuhudiwa baadhi ya maamuzi ya kiserikali yenye wajihi huo yakiendelea kufanya kazi yake.

Chombo hicho kilichoko chini ya uenyekiti wa mwanazuoni bingwa wa sayansi ya siasa, Profesa Rwekaza Mukandala, hadi sasa imeshakusanya maoni kutoka vyama mbalimbali vya siasa nchini, pia watu binafsi.

Suala la maridhiano nchini, kimsingi lina mzizi mrefu. Itakumbukwa mara kadhaa huko nyuma, mwanazuoni na mchambuzi mahiri wa siasa nchini, hasa kwa nyendo za visiwani Zanzibar, Profesa Haroub Othman, amekuwa akihimiza haja ya kuwapo hatua za maridhiano kumaliza mvutano wa kisiasa visiwani, hasa kati ya chama tawala CCM, na CUF.

Marehemu Profesa Othman, msomi wa sheria aliyepatikana katika Taasisi ya Taaluma ya Maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar e Salaam (UDSM), akashauri ikiwezekana hata viongozi wa dini kuhusishwa katika hilo la Zanzibar ambako pia ni kwao.

Hadi sasa, ndiyo hatua iliyofikiwa kwa marekebisho ya Katiba ya SMZ, kuunda serikali ya umoja kitaifa na kugota mvutano, aliyekuwa kiongozi wa CUF wakati huo Maalim Seif Sharrif Hamad kuingia rumande na kwa wakati mwingine, hatua kama hiyo kwa viongozi 18 wa CUF.

Katika sura ya maridhiano chini ya katiba iliyorekebishwa Zanzibar, Maalim Seif kupitia uchaguzi akawa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, baada ya misuguano ya muda mrefu iliyokuwa ikitulia taratibu kwa hatua,

Hadi kufika awamu ya sasa ya siasa za visiwani kuna onekana shwari sana chini ya Rais Mwinyi, kulinganisha na nyuma ilikotoka, hasa mara tu baada ya mageuzi ya kuingia mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992.

Rais Mwinyi amedumu muda mfupi na Makamu Maalim Seif, kabla ya mauti kumkuta, lakini safari iliyopo akipeperusha bendera ya chama ACT Wazalendo, baada ya kujiengua kutoka chama alichoshiriki kukiasisi - CUF, kutokana na misuguano ya ndani.

Simulizi kama hizo za maridhiano zina somo lingine la marejeo nchini Kenya kufikia hali mbaya kitaifa, ikiwamo mauaji, kabla ya kufanyiwa marekebisho ya katiba nchi hiyo ikatulia kisiasa.

Ni hali iliyodumu kupitia serikali ya umoja, sasa kukionekana amani hadi sasa, kipindi kinachoendelea cha mashindano ya kufikia uchaguzi mkuu wa mwezi Agosti mwaka huu.

KUELEKEA UCHAGUZI AGOSTI 9

# Tume yapuliza kipenga

## • Ni mtifuano mkali Raila Odinga Vs Ruto



Raila Odinga



Martha Karua



William Ruto



Rigathi Gachagua

**Na GAUDENSIA MNGUMI**

TUME huru ya uchaguzi na mipaka ya Kenya imepuliza kipenga na sasa wagombea wawili wakuu wa urais nchini humo Wiliam Ruto wa Kenya Kwanza Alliance na mpinzani mkongwe Raila Odinga kutoka Azimio la Umoja, wakiruhusiwa kuanza kampeni.

Wote wawili wamepewa vyeti vya kugombea urais na kuidhinishwa na tume hiyo, Raila anapanda majukwani baada ya kumchagua mtetezi wa haki za wanawake na haki za kijamii Martha Karua kuwa mgombea mwenza.

Wakati mpinzani wake William Ruto, akiingia jukwaa na mwanaharakati stadi wa kisiasa , mfanyabiashara na tajiri Rigathi Gachagua.

Lakini cha kufurahisha ni kwamba wagombea wenza wote ni Wakikuyu, kabila lenye watu wengi zaidi nchini Kenya. Huenda lengo lao ni kwamba Odinga kutoka kabila la Waluo na Ruto ambaye ni Mkalenjini wote wanatoka katika jamii nyingine na wanachohitaji ni kuvutia na kuvuna kura nyingi za Wakikuyu.

Odinga ( 77), alimtaja Martha Karua, aliyekuwa waziri wa zamani wa sheria ambaye alijipatia jina la utani "Iron Lady" kuwa Nibu Rais, akiwa mwanamama wa kwanza kupewa jukumu hilo.

Anampongeza kwa kukabiliana na washiriki wote wanaume katika nyanja ya kisiasa inayotawaliwa na wanaume.

Martha alijitosa kugombea urais mwaka wa 2013 baada ya kuwa mbunge kwa miongo miwili na katika baraza la mawaziri alikuwa Waziri wa Maji, na Waziri wa Sheria kuanzia 2003 hadi 2009.

Odinga alimsifu Karua kwa sifa zake za kuleta mageuzi.

"Baada ya miaka 60 (ya uhuru wa Kenya)... hatuwezi kuendelea na utawala wa kiume wa watendaji wakuu serikalini" .

Ndani ya duru za kisiasa za Kenya, Karua ana sifa ya ukakamavu na ustadi na hapo awali amepuuzilia mbali siasa za Kenya kama "klabu ya wavulana matajiri".

> "Baada ya miaka 60 (ya uhuru wa Kenya)... hatuwezi kuendelea na utawala wa kiume wa watendaji wakuu serikalini".

**KALONZO KUTEMWA**

Hatua ya Odinga ya kumsambaratisha kiongozi wa Wiper Kalonzo Musyoka, alimpa nafasi Martha Karua, ambaye anatarajiwa kutumia mbinu zote kupata kura za Wakikuyu.

Kalonzo amewahi kuwa Makamu wa Rais wakati wa Mwai Kibaki, alikuwa mgombea mwenza wa Odinga katika chaguzi mbili zilizopita na alikuwa miongoni mwa wagombea kadhaa waliotarajiwa kuwania nafasi ya Naibu Rais wa Odinga.

Baada ya kukosa nafasi hiyo alisema atagombea akisimama mwenyewe kama mgombea wa urais, hata hivyo Tume ya Uchaguzi na Mipaka IEBC ilimtosa kutokana na sababu za kiufundi.

**RUTO ANAVYOJITUTUMUA**

Ruto, Naibu Rais wa sasa wa Kenya, alimteua Rigathi Gachagua, kuwa mgombea mwenza ambaye amekaa bungeni kwa kipindi cha miaka mitano sasa akiwa kwenye muhula wa kwanza kutoka eneo lenye wapiga kura wengi chini ya Mlima Kenya, ambako kunaelezwa kuwa ni kitovu cha Wakikuyu wafanyabiashara matajiri.

Iwapo Odinga, atapata nafasi ya kuwa Rais 2022 atakuwa wa kwanza kuvunja mwiko baada ya kabila la Wakikuyu kutoa marais watatu kati ya wanne wa Kenya tangu uhuru ulipopatikana mwaka 1963 kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza.

Marais hao ni Baba wa Taifa Jommo Kenyatta, Daniel Arap Moi, Mwai Kibaki na Uhuru Kenyatta,anayemaliza muhula wake wa pili Agosti , 2022

**WAGOMBEA WENGINE**

Wanaogombea kwa tiketi ya vyama vya kisiasa walioidhinishwa na tume ni pamoja na Gavana wa Murang'a Mwangi Wa Iria kupitia chama cha Usawa Kwa Wote Party, Profesa George Wajackoya kutoka chama cha Roots, Ekuru Aukot muungano wa Thirdway Alliance, Jimi Wanjigi chama cha Safina, Njeru Kathangu wa Ford Asili na David na Mwaura Wahiga wa Chama cha Agano).

Odinga ambaye zamani alikuwa kiongozi mkongwe wa upinzani alijaribu mara nne kugombea urais lakini bila mafanikio anaungwa mkono na Rais aliyemaliza muda wake Uhuru Kenyatta.

Uhuru baada ya kutofautiana na Ruto ambaye ni Naibu wake ameendelea kusisitiza kuwa hafai kuwa rais wa Kenya, taifa lenye uchumi mkubwa zaidi Afrika Mashariki.

Lakini Ruto kwa upande wake anawashawishi Wakikuyu na wapiga kura wengine nchini humo kuwa yeye ni mtu wa mabadiliko akiwaahidi kubadilisha mwelekeo wa uchumi wa serikali kutoka miradi mikubwa ya kazi za umma na kampuni kubwa za serikali na kuurudisha kwa kampuni ndogo zinazomilikiwa na wananchi akitumia jina la "hustlers," au wanaosota.

Uchaguzi wa Ruto kutua kwa Gachagua ni kwa sababu alifanikiwa kukusanya umati mkubwa wa wanachama wa chama chake cha United Democratic Alliance (UDA), katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.

**UCHAGUZI MGUMU**

Mtandao wa Bloombeger Africa Edition, unaeleza kuwa wagombea wakuu Raila na Ruto, wanakaribiana kwenye kinyang'anyiro hicho.

Mtandao unasema kiongozi wa upinzani nchini Kenya Raila Odinga, ambaye anawania urais kwa mara ya tano safari hii , anadaiwa kupewa nafasi kubwa mbele ya mpinzani wake Naibu Rais William Ruto katika kura ya maoni iliyofanyika karibuni Mei 18,2022.

Odinga anapewa nafasi kwa asilimia 39 ya wapiga kura, ikilinganishwa na asilimia 35 ya Ruto. Akiwanukuu watafiti wa mjini Nairobi wa kampuni ya Tifa Research, ilieleza katika taarifa iliyotumwa kwa barua pepe.

Takriban asilimia 14 ya waliohojiwa bado hawajaamua kuhusu chaguo lao, wakati asilimia 9.0 ya wengine hawakutaka kusema mgombea wanayempendelea ni nani, kampuni hiyo ilisema.

***MITANDAO***

## JUKWAA LA UONGOZI

# MEMBE: SIBANDUKI TENA CCM HADI NIFE

### •Nimerudi, sababu zilizoning'oa hazipo tena

**Na Beatrice Shayo**

"DHAMIRA yangu ya kukitumikia chama hadi nitakapokwenda kaburini ipo pale pale. niliondolewa CCM nilisikitika sana... nilisononeka na ninyi mlisikitika na mkasononeka pia."

Ni ushuhuda wa aliyewahi kugombea urais katika uchaguzi mkuu wa 2015 kwa tiketi ya chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe.

Membe mwana CCM mkongwe na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika awamu ya nne, alivuliwa uanachama Februari 2020.

Sababu zikitajwa kuwa uamuzi huo ulichukuliwa dhidi ya kada wake ni kutokana na mienendo yake katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2014.

Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, iliyokutana Februari 28, 2020, iliazimia Membe kufukuzwa uanachama baada ya taarifa ya ndani ya chama hicho kuonyesha mwenendo wake kuanzia 2014 kutoridhisha, ikibainisha kuwa aliwahi kupata adhabu nyingine lakini hakujirekebisha wala hazikumsaidia.

Baada ya kuvuliwa uanachama Julai 15, 2020 alijiunga na ACT-Wazalendo akawa mshauri mkuu na mwishoni aliteuliwa kugombea urais kupitia chama hicho.

Machi mwaka huu Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, ilimsamehe na kumrudishia uanachama baada ya kufuatilia mienendo yake na kuridhika.

Akizungumza wakati akikabidhiwa kadi yake na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, mwishoni mwa mwezi uliopita mkoani Lindi, anasema amefarijika kurejeshewa kadi yake.

"Nimefarijika kati ya Machi 30 na Aprili mosi , mwaka huu niliitwa Dodoma kwenye kamati ya maadili nikapewa nafasi na Rais na Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, nizungumze na wajumbe wa Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa ili nieleze chochote nilichokuwa nacho kuhusiana na kurejea nyumbani,"anasema Membe.

Anamshukuru Mwenyekiti wa Chama kwa kumpatia nafasi ya kuzungumza na kuazimia kwa kauli moja kurejea CCM.

"Nimerejea CCM kwa sababu mbili ya kwanza nilishauriwa na viongozi wa dini kwamba nirejee CCM nilishauriwa na viongozi wa CCM ngazi ya taifa na mikoa nirejee nyumbani , nilishauriwa na marafiki wa bara na visiwani kila aliyeniona , wanachama wa CCM walinishauri nirudi CCM,"anasema Membe.

Kutokana na ushauri wote huo hakuwa na namna nyingine bali ni kutii mawaidha na ushauri wa viongozi wa chama, viongozi wa dini walimweleza, kumuomba na kumshauri arudi CCM amekubaliana na ushauri wao na amerudi rasmi, anaongeza Waziri wa Mambo ya Nje mstaafu .



Bernard Membe.

Anasema sababu ya pili ya kurudi ni kutokana na dhamira yake ya kukitumikia Chama Cha Mapinduzi hadi atakapokwenda kaburini.

"Nilipoondolewa CCM nilisikitika sana nanyi mlisononeka sababu zilizonifanya niondoke CCM hazipo tena Narudia hazipo tena nimerudi namshukuru Mwenyekiti wa CCM na wajumbe wa Kamati Kuu kunirudisha nimerudi kwenye chama ambacho nimezaliwa, kukulia na kusomeshwa," anasema

Anaongezea :"Ninaahidi sitaondoka tena nitabaki CCM hadi mwisho wa uhai wangu. Kurudi kwangu nitaendelea kukitumikia chama changu kushirikiana na mbunge wangu Nape Nnauye. Mwaka 2015 niliahidi kuwaletea Nape nikamleta. Mtama sasa mtakuwa na wabunge wawili mbunge wetu Nape na mimi nitakuwa mbunge wa chini chini."

**SIMULIZI ZA NAPE**

Mbunge wa jimbo la Mtama ambaye pia ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, anasema baada ya Membe kuondoka kwenye chama wananchi wengi walichukia, ingawa aliwaomba wasichukie akiamini ipo siku atarejea.

"Mwenyezi Mungu ametu-rudishia faraja watu wa Londo, Chiponda... Mtama ni wastaarabu na hatuna shida tena, tuna imani kubwa na Membe, alinikabidhi kijiti na kuvaa viatu vyake, kulikuwa na mambo yaliyokwama huku nyuma kwa sababu za kisiasa, lakini Mama Samia amekuja amezion-doa," anasema.

Aidha, alitumia nafasi hiyo kuwataka wananchi wa Mtama kushikamana, fitina ambazo ziliingia kati zimekwisha.

"Membe amenipigania katika mambo mengi, nilipotaka ubunge Ubungo baada ya kuonekana fitna zimeingia katikati Membe aliamua kuchora ramani."

Anaongezea kuwa:"Ndio maana safari yangu ya ubunge imekuwa nyepesi. Kaka Membe amenipigania sana na bahati nzuri amerudi CCM."

**AKABIDHIWA KADI**

Shaka anasema Membe amerudishwa CCM kwa kufuata utaratibu ikiwamo kujadiliwa na tawi lake na vikao vya ngazi ya juu.

Anasema Membe na wanachama wengine zaidi ya 1,670 walivuliwa uanachama wamejadiliwa katika vikao na kurejeshewa uanachama, hivyo wanaweza kukabidhiwa kadi zao kwenye matawi yao.

"Kurejea Membe ndani ya Chama Cha Mapinduzi ni kuendelea kuwa na chachu ya kudumisha umoja na mshikamano hususani kwa wanachama wa jimbo la Mtama,"anasema Shaka.

**AONYA MADIWANI**

Shaka anawataka madiwani wa CCM nchini kuhakikisha wanasimamia maslahi mapana ya wananchi wao hilo ni jambo la msingi.

"Kumekuwa na changamoto kwa ndugu zetu madiwani wanajisahau wakifika huko...alilolieleza wananchi wapo sahihi kwa asilimia 70 wapo baadhi ya madiwani wakifika huko kwenye Halmashauri, majiji, manispaa wanasahau kilichowafikisha huko ni wananchi,"anasema.

Anaongeza kuwa: "Simamieni gharama za miradi na iweze kuwafikia wananchi na manufaa yake yaweze kuonekana yapo maeneo kadhaa madiwani hawatimizi wajibu wao niwaombe madiwani wa CCM kutimiza wajibu wao kwa wananchi."

Shaka anasema mpaka wananchi wanaona udhaifu huo kuna sehemu hawafanyi vizuri na kazi ya kiongozi ni kujitathimini na kuona mambo hayaendi vizuri unajipanga upya.

"Ninyi ndiyo wasaidizi wa Rais Samia, sote tutimize wajibu wetu wa kuwatumikia wananchi hawa wametuweka katika hiyo nafas," anasema Shaka.

Shaka alifikia uamuzi huo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wakilalamikia baadhi ya viongozi kutotoa ushirikiano kwa wananchi licha ya kwamba wao ndiyo wamewaweka madarakani.

"Nikiri kweli kuna tatizo la baadhi ya viongozi lakini tayari hatua zimeshachukuliwa na kuanzia hivi sasa viongozi hawa wanaochaguliwa watapatiwa mafunzo ili wawe na uwezo na ujuzi wa kutosha," anasema.

Mwanachama Mzee Bakari Omar Bakari, anaeleza kuwa kuna tatizo la baadhi ya viongozi wa chama akiwemo diwani wao kupungukiwa na sifa za kiuongozi.

Anasema tatizo la Lindi wana viongozi ambao wamewachagua wakati wa kampeni lakini elimu zao ni ndogo wanatekwa na wakuu wa idara.

"Kila kitu kitakachokuwa kinaulizwa kinahusu elimu bila kuwa na elimu huwezi kuleta maendeleo tujitahidi kupata viongozi wenye elimu ya kutosha ili waweze kututetea wananchi ambao wapo chini kwenye malalamiko mengi ,"anasema Bakari





## Askofu ahamasisha ushiriki sensa ya watu na makazi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Pentecostal Holiness Mission Tanzania (PHMT), Nkumbu Mwalyego, amewaomba viongozi wa dini kuendelea kutoa elimu kwenye nyumba zao za ibada kuhusu umuhimu wa waumini wao kushiriki kikamilifu kwenye zoezi la sensa ya watu na makazi Agosti 23, 2022.

Rai hiyo ilitolewa na askofu huyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye ibada ya kuweka wakfu jengo la kanisa hilo lililopo Makole.

Mwalyego, alisema sensa hiyo itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu viongozi wa dini wana mchango mkubwa kupitia nyumba zao za ibada kuwaelimisha waumini wao ili waweze kushiriki kikamilifu na serikali kufikia malengo yake.

Akizungumza baada ya kufanyika kwa ibada hiyo iliyoambatana na changizo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo hilo, aliwataka Watanzania kujibu kwa usahihi maswali yatakayoulizwa na wataalam wa sensa.

"Mpango wa kuhesabiwa ni wa kimungu hivyo hakuna sababu ya kutoa majibu ya uongo ambayo yanayoweza kuisababishia serikali kushindwa kufikia malengo yake ya maendeleo kwa ajili ya Watanzania wake," alisema.

Aliwataka waumini kuwekeza mali na fedha zao katika huduma za kiroho na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya taifa na kanisa kwa ujumla.

Naye Katibu wa Usharika huo wa kanisa hilo, Mariam Mwiru, akisoma risala alisema jengo hilo linahitaji Sh. 70,000,000 kukamilika.

**Aliwataka waumini kuwekeza mali na fedha zao katika huduma za kiroho na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya taifa na kanisa kwa ujumla.**

# Mabadiliko tabianchi yaathiri mifugo nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki, amesema mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari kubwa kwa wafugaji nchini kutokana na mifugo mingi kufa kutokana na ukame ambao umesababishwa na uhaba wa mvua.

Ndaki, alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua kongamano la wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi linalofanyika jijini hapa kwa siku tatu likiwa na lengo la kujadili athari za mabadiliko tabianchi katika sekta hizo nchini.

"Mwaka jana ng'ombe wamekufa wengi sana, kwa eneo la Simanjiro pekee walikufa ng'ombe zaidi ya 900,000, lakini wengi Morogoro na Pwani na maeneo mengine mengi hadi bei ya nyama ikapanda nikawa naulizwa mimi kana kwamba natembea na mabucha.

"Watu wa Dar ndiyo walikuwa wanapiga kelele kweli waziri nyama inapanda toa bei elekezi, lakini hii inamaanisha kuwa mabadiliko ya tabianchi yalituathiri sana hasa kwenye malisho na maji hali iliyosababisha mifugo kukosa afya na kupoteza ubora sokoni," alisema.

Kadhalika, alisema mabadiliko ya tabianchi hayaathiri sekta ya mifugo pekee bali hata katika sekta ya uvuvi.

"Joto linapoongezeka matumbawe yakipata joto linasababisha hata uzalianaji wa samaki kupungua hivyo mabadiliko ya tabianchi ni moja kati ya sababu kuu inayo athiri sana sekta hizi za kilimo, mifugo na uvuvi," alisema.

Vilevile, alisema mabadiliko ya tabianchi pia yanasababisha uharibifu wa miundombinu ikiwamo barabara na maeneo mengine.

"Mwaka jana kulikuwa na mvua nyingi sana mliona namna ambavyo ilivyo haribu barabara zetu kila mbunge alikuwa analalamika bungeni, lakini tunashukuru sana Rais alitoa kiasi cha fedha kwenda kurekebisha barabara zetu," alisema Ndaki.

Alisema kutokana na hali hiyo ipo haja sasa wafugaji kuanza kuelimishwa namna ya kuanza kukabilina na mabadiliko hayo.

"Lazima tuanze kutafuta namna gani tutasaidia wafugaji wetu kwenye kubadili stadi za ufugaji ili twende sawa na mabadiliko tabianchi, lakini tukiacha hali iendele hivi itakuwa ni shida," alisisitiza Ndaki.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo Dk. Christin Ishengoma, alisema kutokana na mabadiliko tabia nchi wafugaji wasipokuwa makini watajikuta hawana cha kufanya.

Mratibu wa Jukwaa hilo, Prof. David Nyange, alisema mada kuu katika kongamano la mwaka huu ni mabadiliko ya tabianchi yanavyo athiri sekta hizo.

"Mwaka huu tunakwenda kujadili namna ya kupunguza athari na kukabiliana na hayo mabadiliko tabianchi, mwaka huu mvua zilichelewa kumekuwapo na joto kali, lakini mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na vita ya Urusi na Ukraine vimechangia kwa kiasi kikubwa kupanda kwa bei ya vyakula pamoja na pembejeo duniani," alisema.

Vilevile, alisema mabadiliko tabianchi yamekuwa na athari nyingi ikiwamo ukame ambao unachangia kupungua kwa chakula, maji pamoja na malisho ya mifugo hali ambayo inasababisha jamii moja kuwa na migogoro na nyingine.



Makamu Mwenyekiti wa soko la Sabasaba, Kombo Kombo, akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wakati wa mkutano na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru (hayupo pichani), kuhusu kuvunjwa kwa soko hilo ili lijengwe la kisasa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TSC yazindua tovuti kuhudumia walimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Utumishi wa Walimu nchini (TSC), imezindua tovuti mpya yenye uwezo wa kuhudumia walimu 258,291 wa shule za msingi na sekondari ambayo itasaidia kufikisha taarifa mbalimbali za tume kwa wakati tofauti na ilivyokuwa awali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo jijini hapa, Mwenyekiti wa TSC, Profesa Willy Komba, alisema pamoja na kuhudumia walimu, pia wadau wengine wa sekta ya elimu, taasisi, wananchi na taifa kwa ujumla, watanufaika.

"Hivi sasa kila kitu kitakuwa kikienda sawa katika utoaji taarifa, tovuti hii mpya itafanya kazi vizuri," alisema Profesa Komba.

Hata hivyo, kabla ya kuzindua tovuti hiyo, aliwasisitiza maofisa TEHAMA na mawasiliano ya serikali katika uendeshaji wa tovuti pamoja na zana nyingine zote za mawasiliano na jamii, zinapaswa kuzingatia uelimishaji na uhamasishaji wa viwango.

Profesa Komba, alisema ni matumaini yake kuanzia sasa taarifa zote hai zenye tija kwa walimu, wateja, wadau na jamii kwa ujumla zitapatikana kwa wakati zikiwa hai na zenye tija kwa walengwa, ikiwamo huduma muhimu za Tume kupitia tovuti hiyo mpya bila kulazimika kufika ofisini.

"Imeelezwa hapa kuwa tovuti mpya iliyoboreshwa itakuwa chanzo sahihi na bora kwa walimu, wateja na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu kupata taarifa mbalimbali za Tume," alisema.

Katibu wa TSC, Paulina Nkwama, alizitaja baadhi ya changamoto zilizosababisha maelekezo ya Tume kwa Menejimenti kutengeneza tovuti mpya kuwa ni pamoja na tovuti ya awali kutengenezwa kwa teknolojia ya zamani.

"Tovuti kutokuwa na uelewa wa kutosha kwenye masuala ya usimamizi wa tovuti hiyo, uhitaji mkubwa wa kuboresha mwonekano na maudhui ya tovuti, uelewa hafifu na usio fasaha wa namna ya kuandaa na kupandisha taarifa," alisema.

Alisema takwimu na nyaraka mbalimbali kwenye tovuti Maofisa TEHAMA, Habari na Mawasiliano kutokuwa na umiliki wa moja kwa moja hali ambayo ilisababisha changamoto katika kuhuisha taarifa na kufanya maboresho mbalimbali kwa wakati na tovuti kutokidhi mahitaji ya Tume kwa kutokuwa na maeneo ya kutosha kwa ajili ya kuweka taarifa mbalimbali za taasisi.

"Tofauti na tovuti ya awali, tovuti hii mpya ni bora zaidi kwa kuwa inakidhi mahitaji ya Tume kutokana na uwezo wake wa kubeba taarifa nyingi zaidi kwa wakati mmoja," alisema Mkwama.

Alisema maofisa wa TSC (TEHAMA na Mawasiliano ya Serikali) kupitia mafunzo yaliyotolewa wanauelewa wa kutosha katika usimamizi na uendeshaji wa tovuti hiyo inayomsaidia mtumiaji (walimu na wadau wengine wa Tume) kupata viunganishi vya mifumo mingine mbalimbali kwa urahisi.



# TMDA yateketeza tani 10 dawa zilizopita muda

Na Grace Mwakalinga, RUNGWE

TANI 10 za dawa aina mbalimbali zilizokwisha muda wa matumizi zenye thamani ya Sh. milioni 180, zimeteketezwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini baada ya kufanya upekuzi na kuzikamata kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi nyumbani kwa mkazi mmoja (jina limehifadhiwa) eneo la Veta.

Akizungumza wakati wa uteketezaji wa dawa hizo lililofanyika Hospitali ya Igogwe, Mkurugenzi wa TMDA, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, alisema dawa zote zilizotekezwa zilikwisha muda wake wa matumizi.

Alisema dawa hizo zilikuwa zinatibu magonjwa ya aina mbalimbali na kama zingetumiwa na binadamu zingesababisha madhara makubwa kwenye mwili ikiwamo vifo na kuongeza usugu wa ugonjwa.

Pia baada ya kufanya upekuzi na kumkamata mtuhumiwa, dawa zote zilitaifishwa na alifunguliwa mashtaka na mahakama iliamuru alipe fidia ya shilingi milioni tano.

"Tunawashukuru wananchi wa Jiji la Mbeya wamekuwa wakitupa ushirikiano pindi wanapohisi kuna biashara holela ya vifaa tiba au dawa kwenye makazi yao, tulifanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo baada ya wananchi kutupigia simu na kutujulisha kwamba kuna mtu kahifadhi shehena za dawa nyumbani kwake, tulishirikiana na Jeshi la Polisi kumkamata mtuhumiwa na kukiri kwamba dawa hizo zilikwisha muda wake na tulimfikisha kwenye vyombo vya sheria," alisema Mshighati.

Alitaja aina za dawa zilizokamatwa kuwa ni sindano ambazo zinatibu magonjwa ya aina tofauti kama zingetumika zingehatarisha afya za wananchi.

Kwa upande wake, Ofisa wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Hans Cheyo, alisema wanazingatia usalama wa afya za watu na utunzaji wa mazingira wakati wa uchomaji wa taka hatarishi hususani dawa zilizokwisha muda.

Alisema kwa kuzingatia usalama wa watu na mazingira NEMC imekuwa ikisimamia uchomaji wa taka hatarishi kwa kuzichoma kwenye maeneo maalum ambayo hayawezi kuathiri afya za binadamu.



Baadhi ya wataalamu wa kuteketeza dawa wakishusha shehena ya dawa zilizokwisha muda wake, zilizokamatwa nyumbani kwa mtu mmoja ambaye (jina linahifadhiwa), Veta, jijini Mbeya, ili ziteketezwe kwenye eneo maalum la kuchomea lililoko Hospitali ya Igogwe, wilayani Rungwe juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Walalamika kuachwa mpango wa TASAF

Na Grace Mwakalinga, CHUNYA

BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Chunya Mjini, wamelalamikia hatua ya Mfuko wa Mandeleo ya Jamii nchini (TASAF), kufunga mchakato wa kukata rufani kwa kaya maskini ambazo zimekosa fursa ya kunufaika na mpango huo, wakidai kuwa idadi kubwa ya kaya zenye sifa katika kijiji hicho zimeachwa.

Taarifa ya TASAF, kufunga zoezi la kaya maskini kukata rufani ya kujiunga na mpango huo, ilitolewa jana kwa wananchi wa Kijiji cha Chunya Mjini.Diwani wa Kata ya Itewe, Alex Kinyamagoha, alisema ukataji rufani ulifungwa na TASAF na kusababisha waombaji kuendelea kulalamika.

"Tunaiomba serikali kuliangalia upya suala hili la kufunga mchakato wa rufani kwa baadhi ya waliokuwa wanufaika wa TASAF kuondolewa kwenye mpango huo, ukiangalia baadhi ya jamii ni kweli zina hali ngumu sana wanahitaji kuingizwa kwenye mfuko huo," alisema Kinyamagoha.

Baadhi ya wananchi akiwamo Sabina Kalinga, aliyetolewa kwenye mpango huo, alisema uchumi wake ni mbaya na aliutegemea mfuko huo kuendesha maisha yake.

Aliiomba serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma waliondolewa kwenye mpango huo kurejeshwa ili kupata fedha za kuendesha maisha yao, kwa kuwa kwa sasa hali ya maisha imekuwa ngumu hawana shughuli zozote za uzalishaji wanazozifanya kwa kukosa mitaji.

"Kuna wanawake wajane hawana mbele wala nyuma maisha yao ni magumu mno ukiangalia watu wenye ulemavu utalia machozi hawana kitu chochote hata kula yao ni ya shida, TASAF ilitusaidia kupata chochote kitu cha kuendesha maisha yao tafadhali serikali mtusaidie," alisema Kalinga.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Chunya Mjini, Gwakisa Mbamba, alisema wanapokea malalamiko kutoka kwa wananchi waliokosa fursa hiyo wakidai wao ndio wamehusika kuondoa majina yao kwenye mfuko huo.

Ofisa Ufuatilia wa TASAF Wilaya ya Chunya, Fanuel Silikwa, alisema utaratibu uliotumika kuwapata wanufaika wa mpango huo ulitumika kwenye mkutano mkuu wa kijiji ambao ndio walipendekeza majina ya wanufaika.

Alisema wanufaika katika kijiji hicho walikuwa 25 na baada ya wananchi kukata rufani waliongezeka na kufikia 56 kuonyesha jitihada zimefanyika.

# Mil. 100/- kulipa fidia uharibifu mazingira

Na Grace Mwakalinga, CHUNYA

SHILINGI milioni 100 zinatarajiwa kutolewa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kama fidia kutokana na uharibifu wa mazingira, ukataji miti, uchomaji mkaa na uchimbaji wa madini uliofanyika katika Halmashauri ya Wilaya Chunya.

Maelezo hayo yalitolewa juzi na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Tamimu Kambona, alipozungumza na wanahabari na wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari, Mkoa wa Mbeya (MBPC), waliofanya ziara wilaya humo kwa ajili ya kujionea shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Kambona alisema wilaya hiyo imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za uharibifu wa mazingira kutokana na aina ya shughuli za kiuchumi wilayani humo zinazohusisha ukataji miti na uchomaji wa mikaa.

Kutokana na hali hiyo, halmashauri imetunga sheria ili kudhibiti shughuli za uharibifu wa mazingira na fedha hiyo itatumika kama fidia ya kupanda tena miti iliyoharibiwa.

"Sio tu kwamba shughuli za uchimbaji wa madini zinaharibu mazingira, lakini ukweli ni zao la tumbaku ndilo linachangia kuteketea misitu yetu, tumekuwa tukikabiliana nalo kwa kutumia pesa zilizotolewa na TFS kupanda miti, kufidia maeneo yalioharibika kwa kukata miti," alisema Kambona.

Aidha, alieleza mchanganuo na mgawanyo wa pesa hizo kuwa asilimia 70 ya fedha zitatolewa na TFS ndizo huelekezwa kwenye kufidia maeneo yaliyo haribiwa kwa uchimbaji wa madini, ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa na kuchomea tumbaku na kiasi kinacho salia kinaelekezwa kwenye shughuli zingine za maendeleo.

Mtendaji wa Kata ya Sangambi, Ntundu Chapa, alisema kutokana na ukuaji wa uchumi suala na uharibifu wa mazingira limekuwa kwa kiwango kikubwa, lakini wanatumia sheria za vijiji na wilaya kudhibiti suala hilo na katika mwaka wa fedha 2121/2022 zimeripotiwa kesi 30 katika yake na zimeshatolewa uamuzi.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya, (MBPC), Joseph Mwaisango, alisema lengo la ziara hiyo ni kuibua fursa mbalimbali zinazopatikana wilayani humo sambamba na kujua vikwazo wanavyokabiliana navyo wachimbaji wa madini ya dhahabu wilayani humo.



## ACT yataka maslahi ya Muungano yazingatiwe

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar haidai wala haitaki kufanyiwa hisani ndani ya Muungano, bali inataka kuwapo haki na fursa sawa kwa pande mbili zilizoungana.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti juzi katika ziara ya kutembelea majimbo ya uchaguzi ya Ziwani na Ole Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema Zanzibar imekuwa ikikosa haki na fursa nyingi za kimaendeleo kutokana na mfumo wa Muungano uliopo sasa ambao hautoi nafasi kwa Zanzibar kuwa na mamlaka ya kufanya jambo lolote la maendeleo.

Alisema hali hiyo inasababisha Zanzibar kutopiga hatua katika jitihada za kusaidia ustawi wa wananchi kiuchumi na kimaendeleo kwenye nyanja mbalimbali na ACT inataka kuwapo mabadiliko ndani ya Muungano ili kuwa na tija kwa Zanzibar.

Alisema Zanzibar siyo maskini lakini tatizo kubwa ni kuwapo kile alichokiita wizi, ubadhirifu na ubinafsi katika kusimamia masuala mbalimbali ya rasilimali za serikali, jambo ambalo linairejesha nyuma Zanzibar.

Akizungumzia masuala ya kodi, kiongozi huyo wa chama na serikali alisema mfumo unaotumika sasa wa kodi sawa kwa Tanzania nzima, hauwezi kuisaidia Zanzibar hasa kwa vile uchumi wake ni wa visiwa ambao unahitaji kwenda sambamba na hali hiyo kama zinavyofanya nchi zingine duniani.

Akizungumzia kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, alisema chama chake kimepeleka mapendekezo kadhaa ya kutaka mageuzi yafanyike katika maeneo kama vile Tume ya Uchaguzi, sheria ya uchaguzi pamoja na kuondosha masheha katika sheria ya uchaguzi.

Jambo lingine ni kufuta uchaguzi wa kura ya mapema kwa kuwa kura hiyo inatumika vibaya.

Aliwataka Wazanzibar kuelewa kwamba silaha pekee ya kufikia malengo ya chama hicho ya kupigania maslahi ya Zanzibar ni kuendeleza umoja na mshikamano kwa kuwa ndiyo silaha ya mafanikio.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Ismail Jussa Ladhu, alisema Zanzibar inahitaji vijana kujua historia ya nchi yao ili kuendeleza jitihada za chama hicho katika kupigania maslahi ya Zanzibar.

Alisema viongozi waasisi wa kupigania maslahi ya Zanzibar walijitolea na kujitoa bila kujali vyeo ama ubinafsi, jambo ambalo linapaswa kuungwa mkono na wananchi wote licha kwamba wengi wao wameshatangulia mbele ya haki.

# Kamati uvuvi zakumbushwa umuhimu kuhifadhi mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MENEJA wa Hifadhi ya Mnemba na Ghuba ya Chwaka kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu, Omar Hakim Fumu, amezitaka kamati za uvuvi na mazingira kusimamia maeneo ya fukwe za bahari ili kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuwa ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha anaweka mazingira safi na salama muda wote.

Alikumbusha hayo jana baada ya kumaliza kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya fukwe za Matenwe Muyuni kwa kushirikiana na Kampuni ya Uwekezaji ya Kisiwa cha Mnemba pamoja na kamati za uvuvi na mazingira Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Meneja Omar alisema lengo la kufanya usafi ni kuyafanya mazingira ya fukwe kuwa safi na salama ili kuufanya uchumi wa buluu kuwa endelevu kupitia mazingira ya hifadhi za bahari, hivyo kuwa kivutio kwa watalii.

Aliwasisitiza wadau walioajiri katika shughuli za kitalii katika maeneo ya hifadhi za bahari, kuacha tabia ya kutupa taka za plastiki kwa kuwa ni kosa kisheria.

Pia akawataka wananchi kuwa na utamaduni wa kufanya usafi muda wote katika maeneo wanayofanya shughuli zao binafsi katika kuhakikisha na kudumisha usafi katika maeneo mbalimbali ili kuweka mazingira mazuri na afya za binadamu kuwa salama.

Meneja Omar alitoa wito kwa wananchi kuzingatia ujumbe wa Siku ya Mazingira Duniani ambao ni 'Dunia ni Moja Tutunze Mazingira' kwa kuwa mazingira ni uhai, hivyo wahakikishe maeneo ya visiwa na fukwe ni safi muda wote.

"Umuhimu mkubwa unahitajika juu ya kupanda miti na mikoko katika maeneo ya hifadhi za bahari kwa faida ya taifa ili tuendelee kuvuta hewa safi na salama kupitia juhudi ya kulinda na kutunza mazingira kwa ajili ya kuzuia mmong'onyoko wa ardhi," alisema.

Rajab Ali Sudi kutoka Kampuni ya Uwekezaji katika Kisiwa cha Mnemba, alisema wapo tayari kutoa ushirikiano katika kuchangia vifaa vinavyohitajika katika shughuli za usafishaji wa mazingira katika maeneo ya fukwe za bahari kwa ajili ya kuondoa taka za plastiki.

Katibu wa Kamati ya Uvuvi katika Kijiji cha Matemwe, Mshenga Ali Mshenga, aliiomba Serikali kuwapatia vitambulisho vinavyotambulika kisheria kwa lengo la kuchukua hatua dhidi ya wachafuzi wa mazingira katika maeneo ya hifadhi za bahari.




Waziri wa Uchumi wa Buluu Zanzibar, Suleiman Masoud (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar jana, kuhusu Siku ya Bahari ambayo huadhimishwa Juni 8. Kushoto ni Waziri wa Uwekezaji Zanzibar, Mudrik Soraga. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yaona fursa ya kilimo cha viungo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imeanza kuwahamasisha wakulima kulima kilimo cha viungo kutokana na kuwa na soko kubwa kimataifa hasa Ulaya.

Waziri wake, Shamata Khamis Shaame, alibainisha hayo juzi alipojibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad Bakari, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kuwajengea uwezo wakulima wa mazao ya viungo nchini.

Shamate alisema wakulima tayari wamehamasika kulima mazao ya viungo kufuatia taasisi mbalimbali kutoa elimu na kuwapatia mbegu za uzalishaji wake.

Alitumia nafasi kuipongeza Jumuiya ya Ulaya (EU) pamoja na taasisi ya Agro-connection ambao wamefanya kazi kubwa kufika hadi vijijini kutoa elimu ya mazao ya viungo na wakulima kuhamasika kikamilifu.

"Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mikakati ya wizara ni kuona kilimo cha viungo kinaleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya wakulima ikiwamo vijijini ambapo tunashukuru wamehamasika kwa kiwango kikubwa," alisema.

Aliyataja mazao ya viungo ambayo wakulima wameanza kuotesha katika mashamba yao ikiwamo vanila, pilipili manga, uzile na tangawizi ambayo bei yake katika soko la dunia ni nzuri na yenye tija.

Zanzibar katika miaka ya 1960 ilikuwa maarufu kwa kuzalisha na kusafirisha nje ya nchi mazao ya viungo ikiwamo karafuu, pilipili manga, uzile na mbata.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUZANA EMANUEL SHOMARI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1243-0044** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BISHOP KISANJI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2012.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/MBU/RB/528089/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............TEMEKE**
**Kituo cha..... JUMUISHI.... Mkoa... DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi............1056/2022................**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: AMIR ALLY**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA: ALLY AMIRI ALLY**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 23 mwezi 06 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 06 mwaka 2022**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO

---

**RAIBA LOGISTICS TANZANIA LIMITED (COMPANY) NUMBER 138585824**
***In member's Voluntary Liquidation***

**Notice to Creditors.**
***(Under section 343 of the Companies Act, 2002)***

**Call for a meeting of creditors.**

The Liquidator intends to convene a meeting of creditors on 15/6/2022. Given circumstances, the meeting will only be held virtually. That is, no physical meeting will be available.

The main purpose of the proposed meeting is to deliberate on the way forward in the winding up process in view of the available assets and liabilities of the company.

The proposed meeting shall take place virtually on **15/6/2022 at 3pm EAT.**

In case of any query pertaining to the said meeting kindly send them to the liquidator's email via pascal@audaadvocates.com or mshanga3@gmail.com.

Signed.
**Pascal Mshanga, advocate**
The Liquidator
For and on behalf of
Raiba Logistics Tanzania Limited
(In member's Voluntary Liquidation)

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JUMA ISMAILI MKWIZU** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC216ABF CHASSIS NAMBA : LTBPK82B4DLC23017, ENGINE NAMBA: KL157FMI13J22775.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI NAMBA: ARU/ARU/RB/225203/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI.

**CATHOLIC RELIEF SERVICES (CRS)**
WANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI **T198APD**.

CHASSIS NO **9C2JD20106R502166**
ENGINE NO **JC30E86502166**

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI
**ARU/ARU/RB/213812/2022**

---

**FOMU MIRATHI-2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............ILALA**
**Kituo cha..... KARIAKOO.... Mkoa... DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi............116/2014................**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HILDA GODFREY WA KARIAKOO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA: JOHN RICHARD RUPIA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 23 mwezi 06 mwaka 2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 06 mwaka 2022**

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO - ILALA DAR-ES-SALAAM

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT [CAP.117]**

**DEED POLL ON CHANGE OF NAMES**

BY THIS DEED,I,the undersigned, **SALUM AUZEBIO MLAWA of P.O Box....TUNDUMA**,a citizen of Tanzania **DO HEREBY RENOUNCE and ABANDON** the use of my names **JACKSON AUZEBIO MLAWA** appearing in my National Identification Card and in lieu thereof do assume the names of **SALUM AUZEBIO MLAWA** and **THEREBY DECLARE** that I shall in future in all records,deeds and instruments in writing and in all actions,proceedings,dealings and transactions upon all occasions whatsoever use and sign the assumed names of **SALUM AUZEBIO MLAWA** instead of the names renounced.

The reason for the changes is that I want to assume my correct given names as given by my parents.

**AND I HEREBY AUTHORISE** and request all persons to address me by such assumed named instead of names renounced. **SIGNED and DELIVERED** by the said **SALUM AUZEBIO MLAWA** who is Known to me personally / identified......... to me by ............ DEPONENT In my presence this ....22nd....Day of ...November...,2021

**BEFORE ME:**
**NAME :..LEONARD KAZIMZURI**
**ADDRESS:..BOX 245.., TUNDUMA.**
**DESIGNATION :...MAGISTRATE**
**SIGNATURE : ..................**

---

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD**
**COURT BROKER**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 04/07/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA PASSO T 308 DCZ, MALI YA GULLIVER SIMIME BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA UHUMA FINANCIAL SERVICES - DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KHALFAN MKANGARA MAERO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA KLUGER yenye usajili namba **T567 DLP,** CHASSIS NAMBA: **ACU200010108,** ENGINE NAMBA: **2AZ0305998.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/225378/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha HOMBOLO Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 1/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SIMON. M. MKOLA wa DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA STANLEY MANYELEZI MTUNDU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote / maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **21 Mwezi APRIL Mwaka 2022** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 31 mwezi 3 mwaka 2022.**

HAKIMU

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO ITISO DODOMA

---


# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

# KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Washambuliaji Nigeria walijifanya waumini

**ABUJA, Nigeria**

POLISI nchini Nigeria imesema watu wenye silaha walioua zaidi ya watu 20 ndani ya kanisa, walijifanya kuwa miongoni mwa waumini.

Msemaji wa polisi alisema kuwa washambuliaji walilipua vilipuzi ndani ya jengo la kanisa, huku wengine wakifyatua risasi nje ya jengo hilo.

Bado haijafahamika malengo ya mashambulizi hayo yaliyotokea katika mji wa Owo ulioko kusini -magharibi mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, idadi kamili ya watu waliofariki na kujeruhiwa bado haijatolewa.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa nchini humo, imelaani mauaji hayo na kueleza inasikitishwa na shambulio hilo dhidi ya waumini.

Kulingana na taarifa ya msemaji wa katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, iliyotolewa na Mratibu wa shughuli za Umoja huo nchini Nigeria, Mattias Schmale, ametoa wito wa kuwepo kwa utulivu na kuomba wahusika wa shambulio hilo kuchukuliwa hatua za sheria.

## Ndugu wawili familia ya Gupta mbaroni

**DUBAI, UAE**

NDUGU wawili kutoka familia ya kitajiri ya Gupta, wamekamatwa wakiwa Muungano wa Nchi za Kiarabu (UAE).

Serikali ya Afrika Kusini, ilitangaza jana kuwa Atul na Rajesh Gupta, wanashutumiwa nchini Afrika Kusini kwa kunufaika kutokana na mahusiano ya karibu na rais wa zamani wa nchi hiyo, Jacob Zuma.

Mazungumzo ya kuwarejesha nchini humo yanafanyika kati ya maofisa wa nchi hizo mbili.

Ndugu hao hao walitoroka Afrika Kusini baada ya tume ya mahakama kuanza kuchunguza kuhusika kwao katika ufisadi mwaka 2018.

Wanashutumiwa kwa kulipa hongo za fedha ili kupata mikataba minono na kuwa na ushawishi katika uteuzi wa maofisa wa serikali wanaoshikilia nyadhifa zenye mamlaka makubwa.

Familia ya Gupta ilihamia Afrika Kusini ikitokea India mwaka 1993.

Pia wanashutumiwa kwa utakatishaji wa pesa nchini India, ambako maofisa wa kodi walivamia mali zao mwaka 2018, ikiwa ni pamoja na ofisi ya kampuni yao iliyopo katika mji mkuu Delhi.

**Wanashutumiwa kwa kulipa hongo za fedha ili kupata mikataba minono na kuwa na ushawishi katika uteuzi wa maofisa wa serikali wanaoshikilia nyadhifa zenye mamlaka makubwa.**

# Russia yakabidhi miili wanajeshi wa Ukraine

**KYIV, Ukraine**

KULINGANA na shirika la habari la Associated Press, Russia imeanza kuhamisha miili ya wanajeshi waliokufa katika eneo la kiwanda cha chuma cha Azovstal kilichopo katika mji wa Mariupol.

Mapema wiki hii iliripotiwa kuwa serikali ya Ukraine na Russia zilibadilishana kwa mara ya kwanza miili ya wanajeshi wa pande mbili waliouawa, kila upande uliukabidhi zaidi ya miili 160 ya wapiganaji waliouawa katika mapigano.

Ofisa wa mawasiliano katika kiwanda hicho, Anna Golovko, amethibitisha kwamba miongoni mwa wanajeshi hao walifariki ndani ya kiwanda.

''Hapa tunazungumzia takriban wanajeshi 52 waliuawa ndani ya kiwanda makumi ya miili tayari imekabidhiwa kwa serikali ya Ukraine na mchakato wa utambuzi wa mabaki ya miili yao kupitia uchunguzi wa vinasaba (DNA) umeanza," alisema.

Taarifa hii pia imethibitishwa na ndugu wa wapiganaji hao tayari wameipokea miili ya jamaa zao.

Idadi kamili ya watu waliofariki katika eneo la kiwanda hicho cha chuma bado haijulikani.

Rais Zelensky alisema zaidi ya wafungwa wa kivita 2,500 waliochukuliwa katika eneo la Azovstal pia wako bado mikononi mwa Russia, lakini serikali yake inafanya kila iwezavyo kuwarejesha nyumbani.

Russia yakanusha madai ya unyanyasaji wa kingono

Ofisa wa Umoja wa Mataifa, Pramila Patten alisema madai ya unyanyasaji wa kingono uliofanywa na wanajeshi wa Russia nchini Ukraine, unazidi kuongezeka.

Madai hayo yalitolewa katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa juzi na kuibua mabishano makali.

Balozi wa Russia, Vassily Nebenzia awali alikanusha madai ya unyanyasaji wa kingono vilivyofanywa na vikosi vya Russia nchini Ukraine.

Alisema akidai uthibitisho' wa madai hayo.

Lakini madai kama hayo yalikuwa yanazidi kuongezeka kwa mujibu wa Patten.

Hadi kufikia Juni 3, Umoja wa Mataifa ulikuwa umepokea ripoti za madai 124 ya unyanyasaji wa kingono unaohusiana na migogoro kote Ukraine.



Meli za kivita za Russia zikiwa katika bahari nyeusi ambazo zinadaiwa kutumika kurusha makombora katika miji mbalimbali ya Ukraine.
**PICHA: BBC**

# Waasi wa Codeco watangaza kusalimisha silaha

**GOMA, DRC**

WAASI wa kundi la Codeco wametangaza kusitisha uasi baada ya mazungumzo ya amani na serikali.

Taarifa iliyotolewa na jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, limesema makubaliano hayo yalifikiwa Jumatatu baada ya mazungumzo ya makabila mbali mbali katika jimbo la Ituri.

Kiongozi wa kabila la Lendu-ambalo linahusishwa na kundi hilo aliingia mkataba na serikali wa kumaliza uhasama.

"Codeco itaheshimu mchakato wa amani tuna matumaini kwamba kuanzia leo amani itarejea katika jimbo la Goma" alinukuliwa Célestin Tawara ambaye ni mwakilishi wa kabila la lendu katika ripoti hiyo ya jeshi.

Hatua hiyo ilitangazwa wakati mkutano wa wakuu wa kijeshi wa kikanda ukifanyika mjini Goma kuamua kuhusu kuundwa kwa kikosi cha kupambana na makundi ya wanamgambo mashariki mwa nchi hiyo.

Baada ya mkutano huu, wataalamu wa kijeshi wa kikanda wanatarajiwa kuweka sheria, vifaa na muda wa mwisho wa operesheni za kikosi hicho.

Haijafahamika lini kikosi hicho kitaanza operesheni yake dhidi ya makundi ya waasi ambayo yatakataa kuweka silaha chini na kujiunga na mchakato wa serikali wa kuwarejesha katika maisha ya kiraia.

Zaidi ya makundi 100 wakishirikiana na wageni huendesha harakati zao katika majimbo ya Kivu Kusini, Kivu Kaskazini na Ituri.

HABARI MICHEZO

# SERENGETI GIRLS YATINGA BUNGENI YAAHIDI KUTISHA KOMBE LA DUNIA

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

TIMU ya Taifa ya Wanawake chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls, jana ilitinga ndani ya ukumbi wa bunge na kukaa kwenye nafasi za mawaziri upande wa kulia wa spika, kisha nahodha wa kikosi hicho kupewa fursa ya kuhutubia kueleza namna walivyoibuka washindi katika mashindano hayo na mipango yao kuelekea fainali za Kombe la Dunia nchini India Oktoba, mwaka huu.

Kabla ya timu hiyo kuingia ukumbini humo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alimkaribisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), George Simbachawene, kutangaza kutengua kanuni ili kuruhusu wachezaji na viongozi wengine kuingia bungeni, huku akiruhusu wabunge kusimama wakati naye amesimama jambo ambalo kikanuni haliruhusiwi.

Baada ya wachezaji hao kuingia bungeni, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, alilieleza bunge kuwa timu hiyo ya wasichana wa chini ya miaka 17, imefanikiwa kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia yakatayofanyika Oktoba mwaka huu, nchini India.

Alisema timu hiyo iliichabanga timu ya Taifa ya Botswana mabao 11-0, ikaibamiza Burundi 6-1 na kisha kufuzu kwa kwa kuifunga Cameron 5-1.

"Serikali kwa kushirikiana na TFF inahakikisha timu inapatiwa malezi na mafunzo ili kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa. Katika mashindano ya dunia Tanzania itaungana na nchi za Nigeria na Morocco,"alisema.

Aidha, alisema matokeo hayo ni mwendelezo wa jitihada za kuwekeza kwenye michezo zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, na kuwaomba Watanzania kuunga mkono timu hiyo inapojiandaa kwenda kushindania Kombe la Dunia.

Naye, nahodha wa timu hiyo, Noela Patrick, alisema ushindi huo ni wa Watanzania wote kwa kuwa ulisubiriwa kwa muda mrefu na wamefungua njia kwa Tanzania kushinda mashindano mengine duniani.

"Tulishikamana kwa pamoja na tulikuwa na heshima kujenga familia moja na wachezaji na kuweka malengo ya pamoja kama familia na hakika tunamshukuru Mungu malengo yetu yametiamia,"alisema.

Alisema ushindi huo umetokana na chachu kubwa ya Rais Samia, na kwamba ushirikiano wa mamlaka mbalimbali umewasaidia kuibuka washindi na wanamatarajio ya kuleta kombe la dunia nchini baada ya kuwa timu ya pili kufuzu mashindano hayo Tanzania baada ya ile ya Watu wenye Ulemavu.

"Kwa kuwa Rais Samia anaupiga mwingi kwa Tanzania nasi tutakwenda kuupiga mwingi nje ya Tanzania. Kwa kasi ya maandalizi tutakwenda kufanya maajabu India,"alisema Noela huku akishangiliwa na wabunge hao.

MAGONGO...



Watoto wakicheza mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Geita Gold yaonya wanaomtaka Mpole

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Geita Gold imezionya klabu zote zinazomuwania nyota wake, George Mpole, kuwa zitakuwa zinafanya makosa makubwa ya kisheria na kikanuni bila kuwasiliana na klabu kwa sababu ana mkataba wa mwaka mmoja zaidi.

Msemaji wa klabu hiyo, Hemed Kivuyo, amesema wamekuwa wakisikia baadhi ya klabu zikimtaka mchezaji huyo kwa kuongea naye mwenyewe, ambapo amesema zinafanya makosa ya kisheria na kikanuni, kwa kuwa zinapaswa kuonana na klabu hiyo ambayo haijafunga milango kwa yeyote anayemtaka.

"Mkataba wake ulirefushwa msimu huu, viongozi wetu walikaa naye, wakaingia naye mkataba ambao utamalizika msimu ujao, hivyo hapaswi kuzungumziwa na klabu yoyote, si ruhusa kwa sababu ana mkataba. Lakini hii haifungi milango kwa timu inayomtaka kwa kufuata taratibu na kanuni kwa ajili ya kufanya biashara, kama klabu ikija rasmi tutawafahamisha kuwa klabu imekuja kumtaka mchezaji wetu," alisema Kivuyo.

Hata hivyo, alisema hata wao wanahitaji sana huduma ya straika huyo aliyechangia asilimia 60 ya mafanikio ya Geita Gold hadi hapo walipofika, ambaye amekuwa pia na mchango mkubwa kwenye timu ya Taifa, Taifa Stars.

Kuhusu kikosi hicho, Kivuyo alisema tayari kimeshaingia kambini kujiandaa na mechi zinazofuata za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tumeingia kambini kujiwinda na mechi zilizobaki za Ligi Kuu, tutacheza nyumbani na Biashara United, baada ya hapo tutatoka. Lengo letu ni nafasi nne za juu, lakini mpaka ilipofika ligi imekuwa tamu na inazidi kuwa tamu kila inapoelekea ukingoni kwa sababu kila mmoja anasema 'yarabi nafsi yangu', kwani unaweza kukutana na teke la farasi anayetaka kufa. Siku zote teke la mwisho la farasi anayetaka kufa ni ni hatari kwa sababu huwa na nguvu kwa kutaka kujinasua, kwa hiyo kila timu haitaki kushuka, mechi zake zinakuwa ni ngumu sana," alisema.

## Mchengerwa azuia michuano bila kibali

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, amepiga marufuku uendeshaji wa michezo kwenye majimbo na wilaya bila kibali cha serikali na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Akihitimisha mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2022/23, alisema uamuzi huo utasaidia kuratibu michezo mbalimbali na kuwa na utaratibu mzuri.

"Naomba niliarifu bunge hili kuwa hakuna mtu anaruhusiwa kuendesha michezo kwenye jimbo au wilaya bila kibali cha serikali kwa maana ya Katibu Tawala Wilaya na TFF,"alisema.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, wizara itaendelea kuratibu michezo hiyo na ndiyo maana wameanzisha mtaa kwa mtaa kupata vijana wenye vipaji vya michezo na kuwaweka kwenye utaratibu maalum,"alisema.

Aidha, aliwataka ma-DAS kutoa ridhaa kwa mashindano yanayotakiwa kufanyika kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Waziri Mchengerwa aliwatoa hofu wasanii kuhusu mgawanyo wa mrabaha wa fedha zinazopatikana kwa kazi za muziki kutumika kwenye vyombo vya habari na kwingine, huku akiahidi kuponya mioyo ya wasanii nchini, kwa kuleta mageuzi makubwa kwenye kazi mbalimbali.

## Azam FC yaikana Ruvuma Queens

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Azam FC umekanusha taarifa inayosambaa kuwa imeinunua timu ya Ruvuma Queens na wako katika mchakato wa kubadilisha jina hilo ili kutimiza kanuni za Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kanuni iliyowekwa na shirikisho hilo, inazitaka timu zote zinazoshiriki michuano ya kimataifa msimu ujao, lazima ziwe na timu za Wanawake zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake kwa nchi husika.

Kutoka na kanuni hiyo, kumekuwapo na taarifa kwamba viongozi wa 'Wanalambalamba' hao wameinunua timu ya Ruvuma Queens na wako katika mpango wa kubadilisha jina ili kujulikana kama Azam Princess au Queens.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amini 'Popat', alisema hakuna ukweli wowote kuhusu taarifa hizo kwa sababu kwa sasa wanapambana kuhakikisha wanafanikiwa kushinda michezo iliyobaki ili kupata nafasi ya kwenda kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho.

"Hatuna uhakika wa moja wa kushiriki michuano ya kimataifa kama hatutafanya vizuri katika michezo iliyosalia ya ligi kwa kupata alama zitakazotupandisha hadi nafasi ya tatu ambayo tunaweza kwenda kushiriki michuano ya kimataifa," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SALAH AIFUNGUKIA BARCA**
MSHAMBULIAJI wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, amewaambia marafiki wake wa karibu kwamba alikuwa tayari kujitolea kuichezea klabu yake ya Liverpool kwa siku zijazo, lakini kuna uwezekano mkubwa akahamia Barcelona baada ya msimu ujao. ***(Mirror)***

**BALE HATAKIWI SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur haina mpango ya kumsajili nahodha wa Wales, Gareth Bale kwa mara ya tatu kwani winga huyo mwenye umri wa miaka 32, bado anatafakari kuhusu ni wapi atakapojiandaa kwa ajili ya Kombe la Dunia la mwaka huu. ***(Telegraph)***

**MANE AOMBA NYUMBA**
MSHAMBULIAJI wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, amemuomba mchezaji mwenzake wa Liverpool, Thiago Alcantara ambaye ni kiungo wa zamani wa Bayern Munich, kama anaweza kuhamia katika nyumba yake iliyopo mjini Munich mara atakapojiunga na mabingwa hao wa Bundesliga msimu huu. ***(Mail)***

**DE JONG AWINDWA UNITED**
BARCELONA iko tayari kwa mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, kuelekea Old Trafford, lakini klabu hiyo ya Hispania bado haijapokea ofa rasmi kutoka United. ***(Sport)***

**AJAX KWA BERGWIJN**
KOCHA wa timu ya Taifa ya Uholanzi, Louis van Gaal amesema mshambuliaji, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24, anahitaji kuondoka Tottenham Hotspur na kujiunga na Ajax "haraka iwezekanavyo." ***(De Telegraaf via Evening Standard)***

**LIGT ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA wana nia na mlinzi wa Juventus, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22. ***(talkSPORT)***

**NEWCASTLE YATAKA WINGA**
MKURUGENZI wa Michezo wa Newcastle, Dan Ashworth ameripotiwa kuweka kipaumbele mpango wa kumleta winga mpya wa kulia msimu huu, huku mchezaji wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 22, na mshambuliaji wa Watford na Senegal, Ismaila Sarr, 24, wakiwa kwenye orodha yake. ***(Sky Sports)***

**DUMFRIES NI BAYERN, UNITED**
MANCHESTER United na Bayern Munich zinamuwania mlinzi wa Inter Milan, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 26. ***(Calciomercato via Mail)***

**BOTMAN NA MKATABA**
MLINZI Sven Botman mwenye umri wa miaka 22, ambaye amekuwa akihusishwa na kuhamia Newcastle United amesema kuwa AC Milan bado wanaendelea na mazungumzo kuhusu mkataba. ***(Football Italia)***

**BERGWIJN BEI EURO MIL. 30**
TOTTENHAM Hotspur wanataka malipo ya euro milioni 30 ili kumuachia Steven Bergwijn ajiunge na klabu nyingine msimu huu. Mchezaji huyo pia anawindwa na Everton, huku mabingwa wa Uholanzi, Ajax bado wakishughulikia dau lake ***(Fabrizio Romano)***

**TOMKINS AJIFUNGA PALACE**
JAMES Tomkins mwenye umri wa miaka 33, ameripotiwa kusaini mkataba mpya na Crystal Palace. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE, VINICIUS NA HAALAND NYOTA WENYE THAMANI DUNIANI

Wengine walioingia 10-bora ni pamoja na Pedri, Bellingham, Phil Foden, De Jong...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe, Vinicius Junior na Erling Haaland ndio wachezaji watatu wenye thamani kubwa zaidi katika soka la dunia, kwa mujibu wa utafiti wa CIES Football Observatory.

Mbappe anakuja kama mchezaji wa thamani zaidi baada ya kuwa na msimu mzuri akiwa na Paris Saint-Germain, akihusika kwenye mabao 60 (mabao 39, asisti 21) katika michezo 46 kwenye mashindano yote.

Vinicius alishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili akiwa na Real Madrid, wakati Haaland hivi karibuni atahama kutoka Borussia Dortmund kwenda Manchester City baada ya kufunga mabao 86 katika mechi 89 alizocheza Ujerumani.

Mbappe alikataa kuhamia Madrid ili kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na PSG mwezi uliopita, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa na mshindi wa Kombe la Dunia anakadiriwa kuwa na thamani ya euro milioni 205.6.

Vinicius ni wa pili akiwa na thamani ya euro milioni 185.5, huku Haaland akiwa na thamani ya euro milioni 152.9 licha ya kuigharimu City euro milioni 60 kutokana na kifungu cha kuruhusiwa kuondoka.

Wengine kati ya 10 bora ni pamoja na wachezaji watatu wa Barcelona Pedri, Frenkie de Jong na Ferran Torres, Phil Foden na Ruben Dias wa City, Jude Bellingham wa Dortmund na Luis Diaz wa Liverpool.

Utafiti wa CIES unatokana na hatua mbalimbali kama vile umri, thamani ya klabu, kiwango cha uchezaji wa wachezaji na mfumuko wa bei.

Ripoti ya CIES imesema: "Mfano wa takwimu wa kukadiria thamani za uhamisho wa wachezaji kutoka timu za Ligi Kuu tano za Ulaya ulijengwa kutokana na sampuli ya uhamisho wa kulipwa euro 1,790 uliofanywa kati ya Julai 2012 na Januari 2020.

"Uwiano kati ya kiasi kilicholipwa na kinachokadiriwa ni kikubwa zaidi ya asilimia 80. Hii inaonesha kwamba vigezo vinavyozingatiwa vinaelezea zaidi ya nne kwa tano ya mapungufu katika kiwango cha ada zinazolipwa kwa uhamisho ulioujumuishwa katika mfano."

**Hawa hapa ndio wachezaji 10 bora katika soka duniani...**

1. Kylian Mbappe (PSG) Euro Mil. 205.6
2. Vinicius Junior (Real Madrid) Euro Mil. 185.5
3. Erling Haaland (Borussia Dortmund) Euro Mil. 152.9
4. Pedri (Barcelona) Euro Mil. 135.1
5. Jude Bellingham (Borussia Dortmund) Euro Mil. 133.7
6. Phil Foden (Man City) Euro Mil. 124.0
7. Frenkie de Jong (Barcelona) Euro Mil. 112.5
8. Luis Diaz (Liverpool) Euro Mil. 110.1
9. Ruben Dias (Man City) Euro Mil. 109.6
10. Ferran Torres (Barcelona) Euro Mil. 109.5


BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,004,0

MECHI KALI
TANZANIA
VERSUS
ALGERIA
1 | 7.45
X | 3.78
2 | 1.49

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SALAH AIFIKIRIA OFA YA BARCELONA



**LONDON, England**

MOHAMED Salah anafikiria upya kuhusu mustakabali wake ndani ya klabu ya Liverpool baada ya kupata ofa kutoka Barcelona, kwa mujibu wa Mirror.

Baada ya Liverpool kufungwa kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid, ilionekana ishara ya mwisho kwa Sadio Mane pale Anfield.

Uhamisho wa Luis Diaz Januari na viungo wapya waliosajiliwa hapo Anfield ndio sababu ya Mane kutaka kuondoka.

Na huenda si yeye pekee, nyota wa 'Wekundu' hao ambaye ataondoka katika klabu hiyo kipindi hiki cha majira ya joto, kwani Salah naye anaonekana kuwa njiani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, aliripotiwa kuwafahamisha marafiki zake wa karibu kuwa yuko tayari kujitolea kucheza pale Liverpool, huku mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao na mazungumzo ya kusaini mpya yakiendelea.

Lakini gazeti la Mirror limedokeza kwamba, ofa iliyotolewa na Barca ya kumsajili kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu ujao, imemfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri kutafakari upya mpango wake wa kukaa hapo Anfield.

Ikiwa Salah hatathibitisha kuongezwa kwa muda, itazifanya klabu nyingine nazo kujitosa kuwania saini yake akiwa amecheza hapo kwa kipindi cha miaka sita.

# Di Maria: Atabiri PSG kumtimua Pochettino

**PARIS, Ufaransa**

ANGEL Di Maria amesema Mauricio Pochettino atafukuzwa kazi kama sehemu ya "mabadiliko makubwa" pale Paris Saint-Germain kabla ya kuanza kwa msimu ujao.

Pochettino ana mkataba na PSG hadi mwaka 2023, lakini imeripotiwa kwa muda mrefu kuwa kibarua chake kiko hatarini.

Kocha wa AS Roma, Jose Mourinho ndilo jina la hivi karibuni zaidi kuhusishwa na mabingwa hao wa Ligue 1, huku kukiwa na uvumi mwingine kwamba, Zinedine Zidane anaweza kuchukua nafasi hiyo ya Pochettino.

Di Maria amecheza mechi yake ya mwisho kwa wababe wa Paris huku mkataba wake ukiisha mwishoni mwa mwezi huu na winga huyo alipendekeza Pochettino pia anaweza kuondoka.



Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina aliiambia TyC Sports: "Kuna wachezaji wengine ambao bila shaka wataondoka. Kwa upande wangu ilikuwa rahisi zaidi kwa sababu hawakuhitaji kuniongezea mkataba.

"Kwa upande mmoja iliuma na kwa upande mwingine hapana. Niliondoka kwa namna ya pekee sana.

"Upendo wa mashabiki wa PSG, walio nyuma ya goli, ndio jambo gumu zaidi kufikiwa. Nitoke nje, waniimbie peke yangu ni vitu ambavyo vimebaki kwenye kumbukumbu."

Aliongeza: "Inaonekana pia wanataka kocha aondoke. Kutakuwa na mabadiliko makubwa sana, lakini nadhani (Lionel) Messi alijua hili mapema tu.

"Itamsaidia kuwa bora zaidi msimu ujao. Nadhani ataanza vizuri sana kwa sababu aliishia kufunga mabao, kutoa pasi za mabao, kujisikia vizuri na kuzoea mazingira."

Di Maria amekuwa akihusishwa na Juventus na Barcelona baada ya kuwa mchezaji huru.

055,092/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.11/06/22 | 19:00 | Faroe Islands vs Lithuania | 2.31 | 2.90 | 3.30 |
| 02.11/06/22 | 19:00 | Ireland vs Scotland | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 03.11/06/22 | 21:30 | Arsenal Sarandi vs Banfield | 2.70 | 3.05 | 2.65 |
| 04.11/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Bosnia and Herzegovina | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 05.11/06/22 | 22:00 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 3.05 | 3.35 | 2.20 |
| 06.11/06/22 | 22:00 | Girona vs Tenerife | 2.32 | 3.10 | 3.05 |
| 07.12/06/22 | 00:00 | Sarmiento vs Argentinos Juniors | 3.05 | 3.15 | 2.28 |
| 08.12/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Bragantino SP | 2.80 | 3.05 | 2.55 |
| 09.12/06/22 | 02:30 | Tombense MG vs CSA AL | 2.70 | 2.75 | 2.90 |
| 10.12/06/22 | 03:00 | Internacional vs Flamengo | 2.80 | 3.30 | 2.37 |
| 11.12/06/22 | 07:00 | Renofa Yamaguchi vs Fagiano Okayama | 3.05 | 2.95 | 2.44 |
| 12.12/06/22 | 08:00 | Mito Hollyhock vs Montedio Yamagata | 2.60 | 3.10 | 2.65 |
| 13.12/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Omiya Ardija | 2.41 | 3.00 | 3.05 |
| 14.12/06/22 | 19:00 | Colon Santa Fe vs Union Santa Fe | 2.43 | 2.95 | 3.05 |
| 15.12/06/22 | 21:30 | Godoy Cruz vs Racing Club | 2.47 | 3.25 | 2.75 |
| 16.12/06/22 | 22:00 | Vasco da Gama vs Cruzeiro | 2.65 | 2.90 | 2.80 |
| 17.12/06/22 | 22:00 | Sporting Kansas City vs New England Revolution | 2.85 | 3.40 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 08/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:15 | 2239 | Bahrain vs Bangladesh | 1.09 | 6.85 | 29.38 |
| 12:30 | 3369 | Henan Jianye vs Shandong Luneng | 4.33 | 3.54 | 1.70 |
| 13:00 | 1039 | FC Tokyo vs Fuji University | 1.15 | 6.88 | 11.79 |
| 13:00 | 5565 | Seoul E Land vs Jeonnam Dragons | 2.07 | 3.04 | 3.48 |
| 13:00 | 5718 | Yokohama vs Sony Sendai | 1.38 | 4.70 | 7.00 |
| 13:30 | 5897 | Tajikistan vs Myanmar | 1.10 | 7.46 | 17.67 |
| 14:30 | 2319 | Shanghai Shenhua vs Shanghai SIPG | 3.01 | 3.10 | 2.25 |
| 14:30 | 2583 | Dalian Aerbing vs Guangzhou RF | 1.87 | 3.44 | 3.64 |
| 14:30 | 5310 | Chengdu Qianbao vs Beijing Guoan | 4.12 | 3.58 | 1.73 |
| 14:30 | 5687 | Hong Kong vs Afghanistan | 2.84 | 2.94 | 2.45 |
| 15:00 | 4078 | Ghana Youth vs Saudi Arabia Youth | 1.47 | 4.10 | 6.20 |
| 15:00 | 5363 | Thailand vs Maldives | 1.08 | 8.08 | 18.72 |
| 16:00 | 1272 | South Korea U23 vs Thailand U23 | 1.42 | 4.22 | 6.27 |
| 16:00 | 1554 | Turkmenistan vs Malaysia | 4.52 | 3.44 | 1.70 |
| 16:00 | 2768 | Uganda vs Niger | 1.50 | 3.93 | 6.66 |
| 16:00 | 4178 | Vietnam U23 vs Malaysia U23 | 1.31 | 4.70 | 8.03 |
| 17:00 | 1340 | Algeria Youth vs Indonesia Youth | 1.29 | 4.61 | 9.02 |
| 18:00 | 1800 | Kyrgyzstan vs Singapore | 1.22 | 5.67 | 9.57 |
| 18:00 | 1944 | India vs Cambodia | 1.18 | 6.08 | 11.76 |
| 18:00 | 4540 | US Tataouine vs CS Sfaxien | 4.03 | 2.90 | 1.97 |
| 18:15 | 5130 | Kagera Sugar vs Biashara United | 2.28 | 2.70 | 3.70 |
| 19:00 | 1819 | Tanzania vs Algeria | 7.45 | 3.78 | 1.49 |
| 19:00 | 2138 | Estonia U21 vs Croatia U21 | 34.11 | 10.72 | 1.02 |
| 19:00 | 2556 | Moldova U21 vs Switzerland U21 | 9.63 | 5.31 | 1.24 |
| 19:00 | 4074 | Gabon vs Mauritania | 1.65 | 3.48 | 5.64 |
| 19:15 | 3025 | Kuwait vs Indonesia | 1.39 | 3.83 | 8.24 |
| 20:00 | 1117 | IFK Kalmar W vs Rosengard W | 22.73 | 9.88 | 1.05 |
| 20:00 | 2022 | Vittsjo W vs Kristianstads W | 2.70 | 3.43 | 2.28 |
| 20:00 | 2470 | Kopparbergs Go W vs Eskilstuna W | 1.29 | 4.93 | 8.09 |
| 20:00 | 3213 | Djurgaardens IF W vs IF Brommapojkarna W | 1.26 | 5.27 | 8.59 |
| 20:00 | 3920 | Umea IK W vs Linkopings W | 7.45 | 4.51 | 1.34 |
| 20:00 | 5871 | Orebro W vs Hammarby W | 2.60 | 3.73 | 2.24 |
| 20:45 | 2443 | ES Setif vs Paradou AC | 1.53 | 3.68 | 5.70 |
| 20:45 | 3132 | USM Alger vs CR Belouizdad | 1.67 | 3.25 | 5.12 |
| 21:00 | 1342 | Mirassol FC U20 vs Tanabi EC SP U20 | 1.48 | 4.14 | 5.51 |
| 21:00 | 2434 | Desportivo Brasil U20 vs Capivariano SP U20 | 2.79 | 3.08 | 2.40 |
| 21:00 | 4306 | Penapolense SP U20 vs Vocem SP U20 | 1.08 | 8.45 | 17.69 |
| 21:00 | 5289 | Iceland U21 vs Belarus U21 | 1.32 | 4.79 | 7.44 |
| 21:45 | 2593 | Wales vs Netherlands | 6.25 | 4.03 | 1.51 |
| 21:45 | 3401 | Ireland vs Ukraine | 2.34 | 3.04 | 3.19 |
| 21:45 | 4765 | Belgium vs Poland | 1.65 | 3.84 | 4.95 |
| 21:45 | 5345 | Scotland vs Armenia | 1.36 | 4.54 | 8.67 |
| 22:00 | 1837 | Ferro CO vs Boca Juniors | 14.76 | 7.09 | 1.12 |
| 22:00 | 3673 | Benin vs Mozambique | 1.54 | 3.84 | 6.27 |
| 22:00 | 4423 | Sudan vs DR Congo | 3.83 | 3.03 | 2.09 |
| 22:15 | 2783 | Jordan vs Nepal | 1.02 | 10.81 | 34.40 |
| 22:15 | 5669 | Grindavik W vs Augnablik W | 1.42 | 4.53 | 5.72 |
| 23:00 | 2871 | Club Atletico Palmaflor vs The Strongest | 2.76 | 3.38 | 2.26 |
| 23:30 | 4385 | Guayaquil SC vs Olmedo | 2.44 | 2.80 | 3.00 |
| 23:30 | 5269 | Puerto Quito vs Libertad Loja | 2.45 | 2.89 | 2.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SPIKA AITAKA TEMBO WORRIORS BUNGENI, KWENDA POLAND LEO

**Salome Kitomari, Dodoma na Saada Akida, Dar**

WAKATI Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, jana akionyesha kutoridhishwa kwa timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu Wanaume, Tembo Worriors, iliyofuzu Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini Uturuki baadaye mwaka huu, kikosi cha wachezaji 25 cha timu hiyo kinaelekea Warsaw nchini Poland leo kushiriki michuano ya Ulaya, imeelezwa.

Spika alitoa maelekezo kwa timu hiyo kufika bungeni leo, kupongezwa kama ilivyofanyika kwa Serengeti Girls jana ambayo iliingia bungeni na kupongezwa kwa kufanikiwa kufuzu Kombe la Dunia, litakalofanyika Novemba mwaka huu nchini India.

Awali, katika taarifa yake kuhusu Serengeti Girls, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, alisema timu ya Tembo Worriors, nayo ilifanikiwa kufuzu Fainali za Kombe la Dunia kwa Watu wenye Ulemavu zitakazofanyika nchini Uturuki baadaye mwaka huu baada ya kuzichabanga timu ya Morocco mabao 2-1, Senegal 1-0 na Cameroon 5-0.

"Kwa sasa timu hii iko kambini kwa maandalizi ya mashindano ya Kombe la Dunia tangu Februari, mwaka huu, na kwamba serikali inagharamia kambi na matumizi yote kwa timu hiyo,"alisema.

"Nazipongeza timu hizi kwa hatua kubwa walizofikia, nawaomba Watanzania wote kujitoa kwa hali na mali kuzishabikia na kuzitia moyo timu zetu, serikali itaandaa utaratibu kwa Watanzania kwenda kushiriki mashindano haya,"alisema.

Baada ya maelezo hayo, Spika alisema: "Waziri kwenye taarifa yako umesema pia timu ya Tembo Worriors imefanya vizuri wanakwenda kutuwakilisha kwenye Kombe la Dunia, lakini hapa ndani (bungeni) hawajaingia.

"Kwa kuwa nao wanakwenda kuwakilisha nchi kwenye Kombe la Dunia kwa Watu wenye Ulemavu Wanaume, na Serengeti Girls wanatuwakilisha pia na wameingia hapa ndani, na kwa kuwa tunatamani timu nyingi zaidi zipate fursa hiyo, naagiza kesho (leo) Tembo Worriors waletwe humu ndani tuwape pongezi pia,"alisema.

Hata hivyo, wakati Serengeti Girls wanatoka ukumbini hapo, alitangaza kuwa amejulishwa kuwa Tembo Worriors wanaelekea nchi Poland, na kuagiza watakaporejea kama bunge halijaisha waletwe au lijalo la Septemba, mwaka huu.

Hata hivyo, rais wa Shirikisho la Soka la Watu wenye Ulemavu (TAFF), Peter Sarungi, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi cha wachezaji 25 kinaelekea Poland leo kushiriki michuano ya Ulaya baada ya kupata mwaliko huo.

Alisema kikosi chake kimefanya maandalizi mazuri, lakini kimepata pigo kwa nyota wao mmoja, Salim Bakari kuwa majeruhi.

Alisema mikakati yao ni kuhakikisha wanaenda katika mashindano hayo kushinda, lakini kuyatumia vema kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika baadaye mwaka huu nchini Uturuki.

"Safari yetu imekamilika kwa asilimia kubwa na tunatarajia Jumatano (leo), kikosi kitaelekea Poland kwa ajili ya michuano hiyo ambayo ni muhimu kwetu katika maandalizi ya mashindano ya Kombe la Dunia," alisema Sarungi.



Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka, akitoa neno kwa timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu, Tembo Worriors, baada ya kushiriki hafla ya kuiaga timu hiyo inayoelekea nchini Poland leo kushiriki michuano ya Bara la Ulaya, ambayo wataitumia kama maandalizi ya kuelekea Fainali za Kombe la Dunia kwa Watu wenye Ulemavu baadaye mwaka huu nchini Uturuki. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam juzi usiku. **MPIGAPICHA WETU**

# Wadada kutua Ihefu FC

**Na Saada Akida**

KLABU ya Ihefu, imesema iko katika hatua nzuri ya makubaliano na beki wa kulia wa Azam FC, Nicholas Wadada kujiunga na kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa 2022/23.

Wadada amechukua uamuzi huo baada ya mkataba wake na Azam FC kufika tamati mwishoni mwa msimu huu na klabu yake hiyo kumueleza haitahitaji tena huduma yake kwa msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Ihefu FC, Zagalo Chalamila, alisema mazungumzo yanaendelea vizuri na wanamatumaini ya kupata saini ya nyota huyo kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu yao.

Alisema usajili wa beki huyo ni mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Zuberi Katwila katika kuhakikisha wanapambana kufanya usajili mzuri ili kuimarisha kikosi chao kwa msimu ujao.

"Mazungumzo na Wadada yanaenda vizuri, kuna vitu vichache tunaendelea kuongea naye na yakienda vizuri tutakamilisha usajili wake na beki huyo kuja kuitumikia Ihefu FC kwa msimu ujao," alisema Chalamila.

Alisema mbali na nyota huyo pia wako katika mchakato wa kuangalia wachezaji wengine wakati huu wakisubiri ligi kufikia tamati ili kuendelea na mazungumzo nyota wengine kutoka Ligi Kuu.

"Kuhusu benchi la ufundi, bado tunaendelea na Katwila baada ya bodi ya wakurugezi kukaa ma kufikia maamuzi hayo ya kumpa majukumu ya usajili na kuimarisha kikosi chetu kwa msimu ujao," alisema Chalamila.

Alisema msimu ujao hawataki kufanya makosa waliyofanya misimu miwili iliyopita, hivyo watahakikisha wanasajili wachezaji wenye uzoefu mkubwa na kiwango kizuri cha kuleta ushindani katika ligi hiyo.

Michezo
Jumatano Juni 8, 2022
Nipashe



## Mbappe, Vinicius na Haaland nyota wenye thamani

MASTAA MJENGONI...



Wachezaji na viongozi wa Timu ya Taifa ya Soka ya Wanawake chini ya miaka 17, Serengeti Girls, wakiwa wamekaa ndani ya ukumbi wa Bunge upande wanaokaa mawaziri, walipotinga bungeni hapo jana kwa ajili ya kupongezwa kwa kufanikiwa kufuzu Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika nchini India Oktoba mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# SIMBA YATANGAZA SIKU KUTUA KOCHA

●●● Huko Jangwani Yanga waingiza shilingi bilioni 1.7 za usajili wa wanachama kwa mfumo wa...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI uongozi wa Klabu ya Simba ukitaja siku rasmi atakayowasili nchini kocha wao mpya anayekuja kurithi mikoba ya Mhispania Pablo Franco, huko mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, watani zao wa jadi, Yanga wametangaza kukusanya jumla ya Sh. bilioni 1.7 katika mchakato wao wa kusajili wanachama kwa mfumo wa kidigitali.

Simba ambao wameeleza kuwa makini katika mchakato wa kumpata kocha ambaye anakidhi masharti ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), wamesema kocha huyo atatua kabla ya Ligi Kuu msimu huu kumalizika ili kushuhudia kikosi walicho nacho na kuona namna ya kukiboresha.

CAF imeweka masharti kwa makocha wa klabu zinazoshiriki Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika kuwa, Kocha Mkuu anapaswa kuwa na Leseni ya Kitaaluma (Pro -CAF) au angalau Leseni ya (CAF A) huku kocha msaidizi akitakiwa kuwa na Leseni CAF B.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, alisema makocha zaidi ya 100 kutoka sehemu mbalimbali duniani wametuma wasifu wao (CV), kuomba kazi ya kuinoa Simba.

Alisema tayari wiki iliyopita katika kikao cha kwanza cha mchujo kilifanyika na kufanya mchujo ambapo majina 40 yalibaki ambayo yataingia kwenye hatua ya pili kwa ajili ya kupita katika mchujo mwingine ili kubakiza machache kabla ya kumpata mmoja mwenye vigezo vyote.

"Mchakato wa kumpata kocha mpya utakamilika ndani ya wiki mbili na atatua nchini kuangalia mechi za mwisho za Ligi Kuu ili kuona mapungufu na kusimamia usajili wa wachezaji wapya ndani ya kikosi chetu cha msimu ujao," alisema Barbara.

Alisema wametoa nafasi kwa kocha anayekuja awe bora na kufahamu vizuri soka la Afrika ambapo katika majina ya makocha waliomba nafasi hiyo, mmoja ni mzawa ambaye ameondolewa katika orodha kutokana na kutokuwa na vigezo.

"Tumepokea wasifu wa makocha zaidi ya 100 kutoka sehemu mbalimbali duniani ambao wengi wao ni kutoka bara la Ulaya na Amerika Kusini, mchakato wa mchujo unaendelea na tunategemea utakamilika ndani ya wiki mbili zijazo na baada ya hapo kocha atatajwa na kutua nchini kwa ajili ya kuanza kazi rasmi," alisema Barbara.

Kwingineko, upande wa pili katika Klabu Yanga, imetangaza kuwa imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 1.7 kutoka kwa wanachama wake kupitia mfumo wa usajili wa kidigitali.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Masingiza alisema pesa hizo zimepatikana kutokana na wanachama 34,650.

Senzo alisema kuwa mafanikio hayo wameyapata katika kipindi cha miezi sita ambapo haijawahi kutokea kwa klabu yoyote kukusanya kiasi hicho ndani ya miezi hiyo. "Haya ni mafanikio ambayo tumeyapata ndani ya miezi sita, tunawashukuru wenzetu wa KILI NET pamoja na N Card ambao wamehakikisha zoezi letu linakwenda vizuri," alisema Masingiza.

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa KILI NET, Mohamed Saleh, alisema mpaka sasa wamefanikiwa kutengeneza mfumo ambao una uwezo wa kukusanya data zote za wanachama waliosajiliwa pamoja na kuboresha zaidi mfumo wa kusajili.

## Stars ni ushindi tu kwa Algeria leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kinashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kuikaribisha Algeria katika mchezo wa kuwani kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zitakazofanyika nchini Ivory Coast.

Katika mchezo huo mashabiki wameombwa kujitokeza kwa wingi kuisapoti Taifa Stars kwa sababu ni mchezo muhimu kwa Tanzania kupata ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu Afcon 2023.

Akizungumzia maandalizi ya mchezo huo Dar es Salaam jana, Kocha wa Taifa Stars, Kim Paulsen, alisema anaamini kikosi chake kitafanya vizuri kwa kucheza mchezo wa kiushindani ili kupata matokeo mazuri.

Alisema Algeria ni moja ya timu za kiwango cha juu Afrika na ina wachezaji wazuri wenye vipaji ila na wao wamejipanga wakiamini wapo kwenye uwanja wa nyumbani na watautumia vema kupambana kupata matokeo mazuri.

"Tumefanya maandalizi mazuri na tutaingia uwanjani tukijua kuwa timu ya Algeria ni miongoni mwa timu zenye viwango vya juu na kwa kulitambua hilo, tunawaheshimu tukiamini utakuwa mchezo wa ushindani,"alisema Paulsen.

Paulsen alisema amezungumza na wachezaji wake kuwa makini hasa kwenye mashindano makubwa kama hayo kuepuka kufanya makosa madogo kwa kuwa yanaweza kuwagharimu na kuadhibiwa.

Alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri isipokuwa mmoja, Himid Mao ambaye alipata majeraha katika mchezo wa kwanza dhidi ya Niger wakitoka sare ya bao 1-1 wakati huo Algeria yenyewe ikishinda 2-0 nyumbani dhidi ya Uganda.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Hamasa ya Taifa Stars, Hajji Manara amewataka mashabiki wa soka kuweka itikadi za timu zao pembeni na kuungana kusapoti timu ya Taifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >